AMBOLA

SEASON 07

PATRICK C.K

PALE MASHUJAA WANAPOLISALITI TAIFA LAO

MTUNZI: PATRICK.CK



© Patrick C.K., 2020

Simu 0764294499

ONYO

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kupiga chapa, kutafsiri au Kuuza hadithi hii bila idhini ya maandishi kutoka kwa **Patrick C. K.**

KANUSHO

Hii ni riwaya ya kubuni. Haihusiani na tukio lolote la kweli linalofanana nalo.

Majina ya mahali na maeneo halisi yamewekwa kwa lengo kutia ladha ya uhalisia kwa wasomaji wake. Isitafasiriwe tofauti.

ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

Simu ya Israel Maungwana mwenyekiti wa chama cha ukombozi wa Afrika iliita akaipokea.

“Kudo kazi imekamilika? Aliuliza Israel.

“Mkuu,kuna tatizo limetokea. Tumefika kwa wakati mahali ulipotuelekeza lakini mlengwa tumemkosa. Tumeambiwa alikuwa hapa muda si mrefu lakini ametoweka bila kumuaga mtu

yeyote. Tumepekua kila mahali hajapatikana. Mkuu,kwa maelezo tuliyoyapata kutoka kwa watu wake tuliowakuta mahali hapo inaonekana wazi yule jamaa alifahamu kuwa tunakwenda mahali pale akatoweka kimya kimya.” alisema Kudo,kiongozi wa timu ya watu sita waliotumwa kwenda kumuua Julius Mukoke.

“Sawa Kudo. Ondokeni mahali hapo na mkae katika utayari hadi hapo

nitakapowapa taarifa nyingine” alisema Israel na kukata simu.

Israel hakupoteza muda akampigia Dkt Nehemia

“Israel.” Alisema Dr Nehemia.

“Mheshimiwa Rais, kuna tatizo limetokea. Vijana wamefika eneo la tukio lakini mlengwa wamemkosa. Inaonekana alipata taarifa akatoweka. Kuna mtu yeyote ulimweleza kuhusu mpango ule wa kumuua Julius?

“Ndiyo. Nilimjulisha Charles Ombe”

“Huyo peke yake? Aliuliza Israel.

“Ndiyo. Niliona nimjulishe ili afahamu kile kinachoendelea. Nilidhani kama mwenyekiti ambaye anafanikisha jambo letu kubwa alipaswa kufahamu.” Alisema Dkt Nehemia.

“Ulifanya kosa kubwa mheshimiwa Rais. Ilikuwa ni misheni ndogo ya siri na hakuna aliyetakiwa kufahamu

zaidi yetu. Tayari taarifa itafika kwa wajumbe wengine na hiyo haitaleta picha nzuri hata kidogo.”

“Ninamuamini sana Charles, sikutegemea kama angeweza kuvujisha siri hii. Nini unanishauri nifanye?” aliuliza Dkt Nehemia.

“Nothing” alijibu Israel.

“Nothing? Kama Julius amekwisha fahamu kuwa anatafutwa auawe atakuwa ni mtu hatari sana. Vipi kuhusu Charles? Kama amevujisha siri

kwa Julius lazima atawaeleza wajumbe wengine.”

“Tayari ninafahamu unakoelekea mheshimiwa Rais. Wazo lako ni kumuua Charles Ombe.”

“Ndiyo. Ni msaliti. Nilimpa siri kaivujisha. Hatufai. Ni bora tubaki na watu wawili waaminifu kuliko kuwa na jopo la wanafiki” alisema Dkt Nehemia.

“Hapana usifanye hivyo mheshimiwa Rais. Hili jambo linapaswa kushughulikiwa

taratibu. Ninaomba uniachie hili suala la Julius nitalimaliza. Charles usimuulize chochote kuhusu Julius. Kama ukizungumza naye yawe ni masuala ya mpango wetu."

"Una uhakika utampata Julius?

"Ndiyo. Nitasaidiana na wale jamaa wakataokuwa SNSA kumsaka Julius na lazima atapatikana tu. Jambo hili ni dogo sana kwangu halinipi shida. Mheshimiwa Rais nitazungumza nawe tena

kesho” alisema Israel na kukata simu.

ENDELEA S07

Ukimya ulitawala ndani ya chumba, Mathew aliyaelekeza macho yake kwa Regina ambaye alionekana kuzama mawazoni. Mathew akainuka.

“Where are you going?” Aliuliza Regina akimtazama Mathew kwa hofu. Mathew hakumjibu kitu alielekea mlangoni akaufungua.

“Get in” Mathew aliwaambia Gosu Gosu na Ruby waliokuwa nje ambao waliingia ndani haraka haraka. Regina alitetemeka kwa woga baada ya macho yake kukutana na macho ya Gosu Gosu.

“Math….” Regina alitaka kusema kitu Mathew akamzuia.

“Regina nilikupa nafasi ya kujieleza lakini umeshindwa kuitumia. Sasa utazungumza kila kitu mbele yetu sote na kama hutataka kuzungumza tutakuacha humu ndani na Gosu Gosu. Unafahamu nini kitatokea.” alisema Mathew akamtazama Regina aliyejawa na hofu.

“Utazungumza sasa au tutoke nje tukuache uzungumze na Gosu Gosu? Aliuliza Mathew. Regina aliinamisha kichwa chini,

akafumba macho kwa sekunde chache halafu akainua kichwa akamtazama Mathew na kusema.

"*Arlight, let's finish this*"

"*Good*" alisema Mathew na kuketi.

Regina aliwatazama wote mle chumbani akitafuta sehemu ya kuanzia kutoa maelezo yake halafu akakohoa kidogo na kusema.

"William na Mary Zanga wazazi wangu ambao tayari

wametangulia mbele za haki, hawakuwa na uwezo wa kuniendeleza kielimu baada ya kumaliza kidato cha sita. Baba alikuwa mchungaji wa kanisa lakini kwa muda mrefu alikuwa akisumbuliwa na maradhi ya mgongo hivyo hakuweza kufanya kazi zozote ngumu. Sikuwa na akili sana darasani, kuchangia na masahibu yaliyokuwa yanaikumba familia yetu sikufaulu mtihani wa darasa la saba. Ilimlazimu baba

kuwaomba waumini wa kanisa alilokuwa analiongoza msaada ili nikasome shule binafsi. Kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita nilisomeshwa na waumini wa kanisa. Baada ya kumaliza kidato cha sita sikufaulu vizuri hivyo sikufanikiwa kupata mkopo wa serikali.” Regina alinyamaza akameza mate kulainisha koo halafu akaendelea.

“Nilikuwa na ndoto ya kufika chuo kikuu lakini baada ya matokeo ya kidato cha sita

kutoka, niliona ndoto hiyo haitakuwa kweli. Nililazimika kutafuta mfadhili wa kunisomesha chuo kikuu. Nilizunguka sana lakini sikufanikiwa. Nilikata tamaa ya kuendelea na masomo ya chuo kikuu nikaanza kutafuta kazi ili niweze kuisaidia familia yangu. Nilifanikiwa kupata kazi katika kampuni moja ya ujenzi. Kwa kuwa nilikuwa nimesoma kidogo nilipewa kazi ya usimamizi wa vifaa. Siku moja nikiwa kazini nilipata mgeni.

Ulikuwa ni muda wa mapumziko ya mchana. Nilikwenda kumuona mgeni yule nikashangaa baada ya kulikuta gari moja zuri la kifahari. Dereva aliyevalia nadhifu ambaye sikuwa namfahamu alinifungulia mlango akanitaka niingie garini. Mle ndani nilikutana na jamaa mmoja mwembamba mrefu, ambaye alijitambulisha kwangu anaitwa Stanley Mbozi.

“Regina samahani kwa kuja sehemu ya kazi bila taarifa” alisema Stanley.

“Bila samahani.” Nilimjibu.

“Regina nina jambo moja tu limenileta hapa muda huu. Kuna wakati ulikuwa unatafuta mfadhili wa masomo ya elimu ya juu. Ulifanikiwa kumpata?

“Hapana. Mpala leo sijafanikikwa kupata mfadhili ndiyo maana nimeamua kutafuta kazi ya kufanya ili niisaidie familia yangu”

“Bado unahitaji kuendelea na masomo yako? Aliuliza yule jamaa.

“Ndiyo. Bado nahitaji sana kuendelea na masomo. Ni ndoto yangu kubwa kufika chuo kikuu.”

“Vizuri.” Alisema Stanley na kuingiza mkono mfukoni akatoa kadi ndogo akanipatia.

“Nipigie kesho mchana kwa namba hiyo hapo katika kadi nitakupa maelekezo” alisema Stanley. Nilimshukuru nikaagana naye na kushuka

garini. Nilibaki nimesimama nikilitazama gari lile likiondoka hadi lilipotoweka machoni pangu. Niliisoma kadi ile ambayo ilimuonesha Stanley Mbozi ni meneja katika kampuni ya utafiti wa madini. Nilianza kuiona ndoto yangu inakaribia kutimia. Mchana siku iliyofuata nilimpigia simu Stanley kama alivyonielekeza. Alinipa maelekezo ya kukutana naye katika hoteli moja kubwa jioni ya siku hiyo. Nilihitaji ufadhili hivyo nilikuwa tayari

kwa lolote. Nilifanya kama alivyonilekeza jioni ya siku hiyo nilikutana naye katika hoteli ile kubwa ambayo ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kuingia. Nilijitambulisha mapokezi nikapelekwa mahali alikokuwa Stanley. Hakuwa peke yake. Alikuwa na watu wengine wawili. Wote wembamba kama yeye na wote walivaa suti za gharama kubwa. Niliwasalimu nikaketi. Tulianza kwa mazungumzo ya kawaida

nadhani lengo lao lilikuwa kunifanya niwazoee. Lengo lao lilifanikiwa kwani baada ya muda sikuwaogopa tena. Tulikuwa kama watu tuliofahamiana muda mrefu. Tulikula chakula pamoja na baada ya kula ndipo mazungumzo yalipoanza ambayo yalikuwa namna hii.

“Regina kama ulivyoona katika ile kadi niliyokupa jana, kampuni yetu inajishughulisha na utafiti wa madini hapa nchini. Kila mwaka tumekuwa

tunatoa ufadhili wa masomo ya juu kwa kwa vijana wanaotoka katika familia duni. Taarifa zako zimetufikia tukafanya utafiti wetu tukagundua unastahili kupata ufadhili wa masomo ya juu.” Stanley alinyamaza akainua glasi yake ya bia akanywa halafu akaendelea.

“Una vigezo vyote vya kupatiwa ufadhili wa masomo na kampuni yetu lakini ni hadi pale utakapokamilisha masharti yetu”

“Mimi niko tayari kwa masharti yoyote. Ni masharti gani hayo?” Niliuliza haraka haraka.

“Tuna masharti kadhaa. Kwanza mtu yeyote ambaye tunamfadhili lazima afanye kazi katika kampuni yetu.”

“Hilo ni jambo jema sana kwani ajira ni ngumu kupatikana zama hizi”nilijibu haraka haraka.

“Vizuri.” Alisema Stanley akanywa tena funda la kinywaji.

“Sharti la pili, kabla ya kukupeleka chuo kikuu, utalazimika kupelekwa katika kozi maalum ya miaka miwili inayohusiana na masuala ya kampuni yetu pekee. Baada ya kumaliza kozi hiyo na kuhitimu ndipo utakapoendelea na masomo ya chuo kikuu lakini wakati huo ukifanya kazi na sisi. Utakuwa ukisoma huku ukipokea mshahara.” alisema Stanley.

Nilijiona mwenye bahati kubwa katika hii dunia.

Nilimshukuru sana Mungu kwa muujiza ule. Nilikubaliana na masharti yote niliyoambiwa na usiku ule ule nilisaini karatasi mbali mbali. Kutokana na furaha niliyokuwa nayo sikuthubutu hata kusoma nini kiliandikwa katika hizo karatasi. Maandalizi yalianza mara moja kwa ajili ya kuelekea nje ya nchi kuanza kozi ya awali ya masuala yanayohusiana na kampuni ile ya utafiti. Ilikuwa ni moja ya ndoto zangu kusafiri nje ya

nchi. Kila kitu kilichotokea ulikuwa ni kama muujiza kwangu. Mambo mengi yalitokea ndani ya muda mfupi sana. Maisha yangu yalibadilika ghafla.” Regin aliweka kituo kwa sekunde chache.

“Nilisafiri kwenda katika nchi ambayo nilitakiwa kusoma kozi hiyo maalum. Nilipokewa uwanja wa ndege nikachukuliwa kupelekwa katika hoteli moja kubwa ya nyota tano. Nilikaa hapo

hotelini siku tano nikila raha na kupatiwa kila nilichokihitaji. Baada ya siku tano nilipelekwa katika chuo nilichopangiwa kusoma. Nilishangaa baada ya kukuta mazingira ya chuo hicho yakiwa si mazingira ya vyuo niliyozoea kuyaona. Kulikuwa na ukimya mkubwa sana na hakukuonekana wanafunzi wakiwa wamezagaa huku na huko kama ilivyozoelekka vyuoni. Siku hiyo nilikutana na wanafunzi wengine kutoka

nchi mbali mbali za Afrika, Asia na Ulaya. Wote tulishangazwa na mazingira ya chuo kile. Siku iliyofuata ndipo tulipofahamishwa kuwa pale tulikwenda kujifunza ujasusi. Ulikuwa ni mshituko mkubwa sana kwangu. Sikuwahi hata kuiota kazi hiyo. Nilikuwa nikisoma ujasusi katika vitabu na kutazama filamu. Sikuwahi kuota kama siku moja nitasomea kazi hiyo. Nililia sana lakini haikusaidia kitu. Ukiingia mahali pale hakuna

kutoka. Rasmi nilianza mafunzo ya ujasusi. Hayakuwa mafunzo rahisi. Miaka miwili ya mafunzo ilimalizika nikafaulu vizuri. Nilirejea nchini ndipo nilipoufahamu ukweli kuhusiana na kampuni ile ya utafiti wa madini ikijulikana kama Tarmo Minerals research company. Kampuni hii ilisajiliwa kama kampuni ya utafiti wa madini lakini haikuwa ikijishughulisha na utafiti wowote wa madini hapa nchini. Ni kampuni

inayojishughulisha na ujasusi.” Regina alinyamaza akawatazama akina Mathew ambao walikuwa kimya wakisikiliza.

“Lengo kubwa la kuanzishwa kwa kampuni hii ni kuchunguza kile kinachoendelea ndani ya serikali na hasa idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi SNSA.”

“Kwa nini SNSA ichunguzwe? Aliuliza Mathew.

“SNSA ilianzishwa kwa lengo la kufanya kazi za usalama wa nchi kwa siri ndiyo maana ikawekwa chini ya Rais. Kazi yao ni kuhakikisha nchi inakuwa salama kwa kuondoa hatari zote kimya kimya bila wananchi au vyombo vingine vinavyoshughulika na usalama wa nchi kufahamu. Tofauti na malengo ya kuanzishwa kwake, SNSA imegeuka na kuwa kama chombo binafsi cha Rais. Simzungumzii Rais aliyepo madarakani sasa peke yake,

bali maRaisi wote walioitumia idara hii waliigeuza mali yao. Badala ya ulinzi wa taifa imekuwa ikitumika katika kunyamazisha watu hasa wale ambao wanaokwenda kinyume na serikali wakiwamo wakosoaji. Mauji mengi ya kimya kimya yamekuwa yakifanywa na idara hii.”

“Nani walioanzisha hiyo kampuni ya utafiti wa madini ili kuichuguza serikali na SNSA? Aliuliza Mathew.

“Sifahamu mpaka leo hii nani mmiliki wa kampuni hiyo”

“Hujwahikuuliza?

“Hapana, sijawahi kuuliza. Mimi ninapewa kazi ya kufanya na ninaifanya bila kuhoji chochote na huo ndio mkataba wangu na kampuni hiyo ulivyo”

Mathew alimfungua Regina mikono akawa huru.

“Gosh! Mmeniumiza mikono yangu! Alisema Regina lakini hakuna aliyemjali.

“Endelea” alisema Mathew.

“Baada ya kurejea nchini, nilijiunga na chuo kikuu. Nikiwa mwaka wa pili, nilipewa maelekezo ya kuonana na watu kutoka chama cha Ukombozi wa Afrika. Hicho kilikuwa ni kipindi cha uchaguzi wa serikali ya wanafunzi chuoni hapo. Mmoja kati ya wagombea uRais wa serikali ya

wanafunzi alikuwa ni mwanachama wa chama cha ukombozi wa Afrika. Tulifanya kampeni kubwa sana na mgombea yule ambaye ni mwanachama wa chama cha ukombozi wa Afrika akashinda uchaguzi na kuwa Rais wa serikali ya wanafunzi. Huo ulikuwa ni mwanzo wa mimi kuingia katika siasa. Rasmi nikawa mwanachama wa chama cha ukombozi wa Afrika. Nilipewa maelekezo ya kugombea uenyekiti wa tawi la

chama hicho chuoni nikashinda. Niliendelea kuaminiwa hadi nikawa mwenyekiti wa umoja wa vijana wa chama hicho ngazi ya taifa. Baada ya kumaliza chuo nilichaguliwa kuwa naibu katibu mkuu wa chama. Baada ya kuwa naibu katibu mkuu ndipo nikapewa maelekezo ya kufanya na kampuni yangu. Nilitakiwa kuchunguza kila kitu kinachofanywa na chama hicho na kumpa taarifa Lucy Mzumile mke wa Gavana.

Sikuwahi kuhoji taarifa hizo Lucy anazipeleka wapi wala Lucy ni nani katika kampuni ile.” Alinyamaza kwa sekunde chache halafu akaendelea.

“Nikiwa tayari naibu katibu mkuu siku moja tulipokea ugeni. Wageni hao walifanya mazungumzo na mwenyekiti peke yake. Kwa taarifa nilizozipata ni kuwa wageni hao walikuja kuzungumza na mwenyekiti kuhusu mipango ya kukiweka madarakani chama cha ukombozi wa

Afrika. Mwenyekiti wa wakati huo, Dkt Elizabeth Meshack aliukataa mpango huo. Dr Elizabeth hakuwa muumini wa siasa chafu. Siku tatu baadaye Elizabeth alifariki kwa kinachodaiwa shambulio la moyo. Katiba ya chama inatutaka kufanya uchaguzi miezi mitatu baada ya kifo cha mwenyekiti na hapo ndipo alipoibuka Israel Maungwana. Huyu hakuwahi kuwa mwanachama na hata jina lake halikuwemo katika

kumbukumbu za chama. Nimejulishwa huyu alikuwa akiishi nje ya nchi. Zilitengenezwa taarifa akaonekana ni mwanachama wa muda mrefu ila amekuwa akiishi nje ya nchi. Taarifa ilionesha alikidhi vigezo vyote vya kugombea nafasi ya mwenyekiti wa chama. Vikao vyote vya chama vilimpitisha kwa kura nyingi na ulipofanyika uchaguzi alishinda kwa kura asilimia tisini na nane. Baada ya Israel

kushinda nafasi ya mwenyekiti wa chama nilipewa kazi na kampuni yanyu kumchunguza na kuhakikisha taarifa zake zote ninaziwasilisha kwa Lucy. Baada ya kupewa kazi hiyo ndipo nilipoanza kufukunyua mambo ya chama nikagundua uwepo wa mfadhili asiyejulikana. Nilishawaeleza kuhusu jambo hili.”

“Ndiyo. Nakumbuka uliwahi kutueleza” alisema Mathew.

“Niliendelea kutoa kila taarifa niliyoipata kwa Lucy kama nilivyoelekezwa. Miaka miwili kabla ya uchaguzi mkuu, viongozi wa juu tuliitwa na mwenyekiti akatujulisha kwamba chama kitasimamisha wagombea katika nafasi ya Rais na wabunge hivyo tuanze maandalizi. Alitueleza kwamba kulikuwa na mpango unaitwa Tanzania mpya. Mpango huo malengo yake ni kukiondoa madarakani chama kinachotawala na kukiweka

madarakani chama chetu cha ukombozi wa Afrika.
Alituweka wazi kwamba katika mpango huo hatutakuwa peke yetu kuna mtandao wa watu wenye nguvu tutashirikiana nao. Niligundua watu wale waliahidiwa fedha nyingi mno kutoka nje ya nchi kama wangefanikisha kukiondoa madarakani chama kinachotawala. Nilipewa maelekezo na kampuni yangu kuhakikisha ninachunguza na kuwapa kila taarifa ya mpango

wa Tanzania mpya. Nilipewa maelekezo ya kumchunguza kwa kina Israel Maungwana. Kama nilivyowahi kuwaambia Israel hapendi ukaribu na watu, nililazimika kumtumia dereva wake anisaidie kumchunguza. Nahisi aligunduliwa kuwa anamchunguza mwenyekiti akaanza kufuatiliwa na akagunduliwa anawasiliana nami. Nadhani hapo ndipo ulipofanyika mpango wa kutuua sote wawili.

Niliwadanganya kuhusu mpango wa kutaka kuhama chama na kuhamia chama tawala. Sina mawasiliano yoyote na kiongozi yeyote wa chama tawala na wala sikuwa na mpango wa kuhama chama. Mimi mwenyewe sikufahamu kuhusu mpango wa kuniua. NInawashukurukwa kuniokoa" alisema Regina na kushusha pumzi akamtazama Mathew.

"Nini kilifuata baada ya kufika Dr es salaam?

Uliwasiliana na kampuni yako? Mathew aliuliza.

“Ndiyo. Nilikwenda kwa Innocent Sungura. Yule ni mmoja wa watu wetu hivyo nilikwenda kwake nikapewa simu kwa ajili ya kuwasiliana na viongozi wangu.”

“Walikuambia nini? Aliuliza Mathew.

“Nilipewa maelekezo ya kutulia na kufuata kile nitakachoelekezwa lakini niendelee kuwachunguza na

kumpa Lucy kila taarifa ya kile nitakachokipata.”

“Regina pamoja na maelezo yako marefu lakini tunapata ugumu kukuamini. Awali ulitueleza ulikuwa na mawasiliano na vigogo kutoka chama tawala na ulikuwa na mipango ya kuhamia chama hicho ndiyo maana chama chako kinataka kukuua. Leo unabadilika na kukiri ulitudanganya. Unatupa ugumu kukuamini” alisema Mathew.

“Ni kweli niliwadanganya baadhi ya mambo and I’m sorry for that lakini haya ninayowaeleza sasa ni ukweli mtupu.”

“Ulimpa Lucy taarifa zetu. Unafahamu mahali alikokuwa anazipeleka? Aliuliza Mathew.

“Sifahamu alikuwa anazipeleka wapi. Maelekezo niliyopewa ni kumpa yeye kila taarifa nitakayoipata”

“Unamfahamu Julius?

“Julius? Regina aliuliza.

“Ndiyo unamfahamu? Yumo katika mtandao wenu”

“Hapana simfahamu” alijibu Regina.

“Kwa nini usimfahamu wakati mko naye katika mtandao mmoja?

“Simfahamu. Ngoja niwaeleze namna tunavyofanya kazi yawezekana mkanielewa. Ni kweli sisi na akina Bernadetha ambao wanajiita Kamati maalum ya Tanzania mpya tuna mashirikiano lakini tumegawana majukumu. Sisi

tumeachiwa jukumu la kuhakikisha mambo ndani ya chama yanakwenda vizuri ikiwa ni pamoja na kumpata mgombea uRais ambaye ana sifa zinazotakiwa. Kazi ya kuandaa na kufanya kampeni tumeachiwa sisi chama lakini masuala yote ya kuhusiana na uchaguzi na namna tutakavyoshinda wanashughulikia kamati hiyo maalum.”

“Nani na nani wamokatika kamati hiyo maalum? Aliuliza Mathew.

“Ni siri. Ndani yake kuna vigogo wakubwa ndiyo maana hawataki kujulikana. Ni siri yao sisi hatujashirikishwa kuwafahamu”

“Bado kuna ukakasi kuhusu sababu ya wenzako kutaka kukuua. Maelezo uliyonipa bado mepesi sana. Ninasema hivyo kwa sababu mpango wa kukuua uliandaliwa kwa umakini mkubwa na kwa

gharama. Wangeweza kukuua kwa namna yoyote ile wanayoweza lakini waliamua kuingia gharama na kumtumia Gosu Gosu kufanya mauaji hayo. Kuna kitu hapa bado hujatuweka wazi. Tueleze tuelewe tafadhali" alisema Mathew.

"Ninachoamini mimi sababu kubwa ya kutaka kunia ni baada ya kugundua ninamchunguza mwenyekiti kwa kumtumia Amani yule

dereva wake aliyeuawa kule Arusha.”

“Kama waliweza kugundua mawasiliano yako na Amani, basi wangegundua pia mawasiliano yako na Lucy lakini mpaka leo Lucy bado yuko hai.”

“Simu yangu imewekewa ukuta maalum hivyo si rahisi kufuatiliwa. Watakuwa walimgundua Amani na wakaanza kumfuatilia. Kuna siku aliwahi kunipigia simu akaniambia kwamba mmoja

wa walinzi wa mwenyekiti alimgundua akiwa amejibanza katika kona ya moja ya jengo akimpiga picha mwenyekiti wakati akizungumza na kigogo Fulani. Anadai kuwa alimpa pesa mlinzi huyo ili asimweleze mwenyekiti. Nadhani kuanzia hapo ndipo alipoanza kufuatiliwa wakagundua alikuwa anawasiliana nami na wakapanga kutuua sote wawili" alisema Regina.

"Bado kuna kitu tunakikosa hapa kuhusu sababu ya

kutakiwa kuuawa. Ulifahamu chochote kuhusu kuuawa kwa yule mtu aliyewekwa na Gavana kukufuatilia?

“Sikufahamu kuhusu mipango ya kuuawa kwake” alijbu Regina.

“Lakini ulifahamu kama alikuwa anakuchunguza? Aliuliza Mathew.

“Ndiyo niliambiwa na Lucy kuna mtu ametumwa kunichunguza”

“Wapelelezi wengine wawili waliowekwa na Gavana kukuchunguza kabla ya huyu wa sasa nao pia waliuawa. Ulifahamu kuhusu wao pia kukuchunguza? Aliuliza Mathew.

“Ndiyo. Kila alipowekwa mpelelezi wa kunichunguza Lucy alinifahamisha na hata pale walipouawa nilijulishwa pia”

“Nani anawaua wapelelezi hao?

“Lucy hutoa taarifa kwa mtandao wa akina Bernadetha ambao huwatumia watu wao kuwamaliza hao wapelelezi” alijibu Regina.

“Nataka kufahamu kwa nini akina Bernadetha wamuue mtu yule pamoja na wapelelezi wengine ambao wanautafuta ukweli kuhusu kupotea kwa Kelvin Mzumile? Kitu gani ambacho hamtaki kujulikane kuhusu Kelvin? Kuna mahusiano yoyote kati ya hiki kinachoendelea sasa na Kelvin

Mzumile? Ninauliza hivyo kwa sababu sioni sababu kwa nini mpelelezi yule auawe kwa sababu yeye alikuwa anakuchunguza wewe na hahusiani chochote na mpango wa Tanzania mpya.”

“Sifahamu sababu kwa nini wapelelezi wale huwa wanauawa lakini nahisi wanahofu pengine wapelelezi hao kama wangeendelea kunichunguza wangeweza kufahamu kuhusiana na mipango yetu ndiyo maana kila

anapotumwa mpelelezi kunichunguza lazima auawe”

“Regina bado kuna mambo unatuficha hutaki kuweka wazi. Suala la wewe kutakiwa kuuawa bado lina elea. Tuliweke hilo pembeni tutaendelea nalo baadaye. Nataka kufahamu kitu kingine. Ulimpigia simu Lucy ukamtaka amjulishe mtu Fulani asifike msibani kwa kuwa sisi tutakuwepo hapo tukifanya uchunguzi. Nani ulitaka taarifa zimfikie ili asifike msibani?

Mathew aliuliza. Ilimchukua Regina sekunde kadhaa kujibu.

“Ni Israel Maungwana”

“Ulifahamuje kama Lucy ana mawasiliano na Israel Maungwana? Kwa nini usingempigia Israel wewe mwenyewe ukamweleza kuwa yuko katika hatari? Kwa nini hukutaka tugundue mawasiliano ya Israel Maungwana na Bernadetha? Mathew aliuliza maswali mfululizo.

Regina alibaki kimya hakujibu kitu. Ruby alipiga hatua kuelekea mlangoni ambako alikuwa amesimama Jombaa.

“Regina uliniambia ulipewa maelekezo ya kumpa taarifa Lucy lakini ulituambia kuwa hujui ni wapi Lucy alikokuwa anazipelekea taarifa hizo. Sekunde chache zilizopita umetueleza kuwa ulimpigia simu Lucy ili amweleze Israel Maungwana asifike msibani. Ulijuaje kama Lucy

anawasiliana na Israel Maungwana? Kwa nini hukutaka tujue kama Israel na Bernadetha ni washirika? Aliuliza Mathew halafu Ruby akamsogelea akamnong'oneza kitu.

"Regina ninakupa dakika kumi za mapumziko. Baada ya muda huo nitakuja kuzungumza nawe tena" alisema Mathew na kumtaka Gosu Gosu kumfunga Regina mikono kisha wakatoka wote.

“Kuna nini Mathew? Mbona tumemuacha yule mwanamke? Aliuliza Gosu Gosu.

“Lucy amezinduka. Tunatakiwa kumuhoji tusikie upande wake na kulinganisha maelezo yake na ya Regina. Kuna kitu tunakikosa kwa Regina. Kuna mambo hataki kuyaweka wazi” alijibu Mathew.

“Mathew ungeniacha niseme naye. Hadi mtakapomaliza kumuhoji Lucy

nina uhakika Regina atakuwa amefunguka kila kitu.” Alisema Gosu Gosu.

“Utapata nafasi ya kuzungumza naye, kwa sasa ngoja tumpe nafasi ya dakika chache ajitafakari. Kuna mambo ameyasema yanaonekana ni ya kweli ila kuna mambo bado anayaficha. Ruby utaifanyia uchunguzi kampuni hiyo ya utafiti madini ya Tarmo. Tunahitaji kuifahamu kiundani kuthibitisha kile alichotueleza

Regina.” Alisema Mathew wakati wakielekea katika chumba alimo Lucy.

Jombaa aliwafunguliwa mlango akina Mathew wakaingia ndani. Lucy tayari alikwisha zinduka. Alikuwa amekaa sofani akionekana kuchanganyikiwa baada ya kuzinduka na kujikuta mahali pale ambako hakujua ni wapi. Machozi yalimtoka baada ya kumbu kumbu kumrejea na kugundua alikuwa ametekwa. Akina Mathew walipoingia mle

ndani, walizidi kumuogopesha. Mathew alivuta kiti akaketi. Gosu Gosu na Ruby wao walikaa juu ya meza. Kwa sekunde kadhaa wote watatu walimkazia macho Lucy. Aliogopa.

“Habari yako Lucy” alisema Mathew. Lucy alitetemeka mwili.

“Kuna chochote unahitaji Lucy, maji au kinywaji chochote?” aliuliza Mathew. Lucy alitikisa kichwa ishara kuwa hakuhitaji kinywaji

chochote,badala yake alijikaza na kuuliza.

“Ninyi ni akina nani?” Sauti yake ilionesha bado alikuwa katika mshituko mkubwa.

“Ninaitwa Mathew Mulumbi. Wenzangu ni Papi Gosu Gosu na Ruby” alisema Mathew na kumtazama Lucy ambaye macho yalimtoka pima. Hakutegemea kuyasikia majina yale mahali pale. Pamoja na mshituko alioupata lakini alijitahidi na kuuliza.

“Kwa nini niko hapa? Ninyi ni askari?

“Sisi si jeshi la polisi lakini tunafanya kazi ya ulinzi na usalama wa nchi kwani hili ni jukumu la kila raia. Tumekuleta hapa kuna mambo machache tunataka kuzungumza nawe halafu tutakurejesha nyumbani kwako. Hatutaki kuchukua muda wako mwingi tunafahamu uko katika kipindi kigumu cha kupotelewa na mume wako hivyo

tunachokitaka kutoka kwako ni ushirikiano. Kama ukitupa ushirikiano na kujibu vizuri kila tutakachokuuliza basi hatutachukua muda mrefu lakini kama ukitudanganya yawezekana usitoke mahali hapa.” alisema Mathew.

“Nini mnakitaka kutoka kwangu hadi mkanileta mahali hapa? Kwa nini msingeomba nafasi tukakaa na kuzungumza nikawaeleza kile mnachokitaka badala ya kutumia nguvu kuniteka na kunileta hapa?

Hamjui mimi ni mke wa Gavana? Naombeni mnieleze haraka sana kile mnachokitafuta kwangu halafu mniache niende zangu vinginevyo mtakuwa mnajitafutia matatizo makubwa.” Alisema Lucy. Mathew alimnong’oneza Ruby kitu, akatoka na baada ya dakika mbili akarejea akiwa na kompyuta yake akampatia Mathew ambaye moja kwa moja alimsogezea Lucy.

“Huyu mwanamke pichani unamfahamu? Aliuliza Mathew. Katika kioo cha kompyuta kulikuwa na picha ya Regina. Lucy aliitazama picha ile na kutikisa kichwa.

“Hapana simfahamu huyu mtu” alijibu Lucy.

“Tazama tena. Una uhakika humfahamu huyu mtu? Hujawahi kuonana naye? Mathew aliuliza tena. Lucy aliitazama tena ile picha kwa makini na kusema.

“Huyu mtu simfahamu lakini picha hii nimeikumbuka. Huyu mwanamke ni yule anayetafutwa na jeshi la polisi kwa tuhuma za mauaji jijini Arusha. Picha yake imesambaa sehemu mbali mbali akitafutwa” alijibu Lucy.

“Ni kweli mwanamke huyu anasakwa na jeshi la polisi kwa mauaji. Nakuuliza kwa mara nyingine tena.Una uhakika hufahamiani na huyu mwanamke?” Mathew aliuliza.

“Hapana sifahamiani naye” alijibu Lucy.

“Labda nikusaidie kidogo. Huyu mwanamke anaitwa Regina William Zanga. Ni naibu katibu mkuu wa chama cha ukombozi wa Afrika. Ni kweli ana tuhuma za mauaji lakini hakufanya mauaji hayo kama inavyodaiwa. Ni yeye aliyetakiwa kuuawa. Mimi na wenzangu hawa tuliomuokoa. Baada ya kumuokoa tulimuondoa Arusha na kumleta Dar es salaam na

kuanza kuwasaka watu wanaotaka kumuua. Wakati tukiendelea kuwasaka watu aliodai ndio waliotaka kumuua, tulibaini Regina ana simu ambayo amekuwa akiitumia kwa uficho.” Lucy macho yalimtoka baada ya kusikia kuwa Regina aligundulika kuwa na simu.

“Tulipata simu hiyo, tukaifanyia uchunguzi ambapo tulibaini Regina amekuwa akiwasiliana na namba moja

tu. Tulipoichunguza namba hiyo tulibaini ni namba yako”

“Sijawahi kuwasiliana na huyu mtu na wala simfahamu. Nitawezaje kuwasiliana na huyu mhalifu? Mmekosea kufanya uchuguzi wenu. Rudieni tena na mtampata mtu aliyekuwa anawasiliana na huyu mhalifu lakini si mimi” alisema Lucy.

“Lucy naomba uwe mkweli tafadhali kwani ukweli pekee ndio utakaokuondoa mahali hapa. Tunao ushahidi wa

kutosha kuwa unawasiliana na Regina.” Alisema Mathew akageuka na kuchukua karatasi ambayo ilionesha mawasiliano yote ya Regina na Lucy.

“Hebu ipite karatasi hii halafu ukane tena hujawahi kuwasiliana na Regina” alisema Mathew. Lucy aliishika karatasi ile huku mikono ikimtetemeka. Hakumaliza kuipitia ikamponyoka.

“Mama unakana tena kwamba hujawahi kuwasiliana na Regina? Aliuliza Mathew.

Lucy hakumjibu kitu alitazama chini.

“Vizuri sana. Sasa tuanzie alfajiri muda mfupi kabla ya Gavana wa benki kuu hajatekwa. Ulipokea ujumbe kutoka kwa mtu anaitwa Julius ukikujulisha kuwa Bernadetha amefariki dunia. Ulimpigia simu huyo Julius na dakika chache baadaye ulimtumia tena ujumbe mwingine mfupi *He’s on move*. Huu ni wakati ambao Gavana aliondoka kuelekea katika ibada ya

asubuhi. Hakufika kanisani alivamiwa akatekwa.” Mathew alinyamaza na kumtazama Lucy ambaye bado alikuwa anatazama chini.

“You sold your own husband.” Alisema Mathew na mara Lucy akainua kichwa. Kauli ile ilionekana kumchoma akasema.

“Siwezi kufanya kitu kama hicho. Yule ni mume wangu na siwezi katu kumuuza kama unavyodai”

“Muda mfupi baada ya Gavana kutekwa ulitumiwa ujumbe na Julius wenye maneno matatu *we have him*. Unakumbuka kile ulichojibu? Aliuliza Mathew. Lucy hakujibu alibaki kimya.

“Nakuuliza Lucy unakumbuka kile ulichomjibu Julius?

Lucy aliendelea kutazama chini.

“Nafsi inamchoma kwa kile alichokifanya kwa mume wake. *What kind of a woman are*

you?” Aliuliza Gosu Gosu huku akiinuka na kumsogelea Lucy.

“Nioneshe kidole chako ulichovaa pete ya ndoa!” Alifoka Gosu Gosu. Mathew hakusema kitu alisimama pembeni akamuacha Gosu Gosu azungumze na Lucy kwa sekunde chache. Lucy hakufanya kile alichotakiwa kukifanya. Gosu Gosu alimvuta mkono na kuiona pete ya ndoa kidoleni.

“Bado una pete ya ndoa kidoleni ambayo alikuvisha

mwanaume uliyemtoa kafara” alisema Gosu Gosu na mara Lucy alijikuta sakafuni baada ya kunaswa kofi zito. Alihisi dunia inazunguka.

“Ahsante Gosu Gosu kwa salamu hiyo. Nadhani tayari Lucy amekwisha fahamu hapa yuko mahali gani” alisema Mathew na kumsaidia Lucy kunyanyuka akaketi sofani.

“Lucy hatuna haja ya kukuumiza lakini tunataka utusaidie kutueleza ukweli. Tunataka kuwafahamu watu

unaoshirikiana nao. Tunataka kumuokoa Gavana kutoka katika mikono ya hao jamaa.” Alisema Mathew. Lucy alifuta damu mdomoni.

“*Who is Julius?* Aliuliza Mathew. Lucy bado alikuwa kimya. Hakuonekana kuwa tayari kusema chochote.

“Lucy umeshiriki katika mpango wa kumteka Gavana wa benki kuu. Ni kosa la jinai. Kama utashindwa kutoa ushirikiano kwetu ili tufahamu mahali alipo Gavana,

tutakukabidhi kwa jeshi la polisi ambako utafunguliwa mashitaka kwa kushiriki katika kutenda kosa hilo la utekaji. Lucy ninakupa nafasi ya kulimaliza suala hili kimya kimya bila mtu mwingine yeyote kujua. Je utatueleza mahali alipo Gavana au tuwasiliane na jeshi la polisi? Aliuliza Mathew. Lucy alimtazama kisha akasema.

"Go ahead. Call them" alisema Lucy. Mathew alimtazama kwa hasira.

“Go ahead. Call police!” Alisema Lucy. Bado Mathew aliendelea kumtazama kwa hasira.

“Kwa nini unashindwa kuchukua simu yako na kuwapigia polisi? Kwa nini hamjawapa polisi ushahidi wa mawasiliano yangu kuwa nilihusika katika mpango wa kumteka Gavana? Mnaogopa nini?” Aliuliza Lucy.

“Well. Tuliweke pembeni suala la jeshi la polisi. Tutalimaliza suala hili sisi

wenyewe” alisema Mathew na kuwaita nje Gosu Gosu na Ruby.

“Huyu mwanamke si rahisi kufunguka kwa kumuhoji kama alivyofunguka Regina. Gosu Gosu ninakupa dakika kumi, zungumza naye. Nitakaporejea hapa Lucy awe tayari kutoa ushirikiano.” alisema Mathew. Gosu Gosu aliingia ndani ya kile chumba akamtazama Lucy kwa hasira.

“Usiku huu mwenzako Regina nusura anitoe uhai.

Nimekasirishwa sana na kitendo kile lakini sijapata nafasi ya kumuonesha mimi ni mtu wa aina gani. Hasira zangu nitazimalizia kwako kwani wewe nawe ni msaliti kama yeye. Ninawachukia mno wasaliti kama ninyi.” alisema Gosu Gosu.

“Twende kwa Regina. Tumuache Gosu Gosu aifanye kazi yake.” Mathew alimwambia Ruby.

“Mathew nina hofu na Gosu Gosu, tukimuacha peke yake

anaweza kuua. Ana hasira sana kutokana na kitendo alichofanyiwa na Regina” alisema Ruby.

“Lucy hawezi kufunguka kirahisi na sisi hatuna muda wa kupoteza. Ngoja Gosu Gosu aseme naye kidogo.” alisema Mathew. Moja kwa moja waliingia katika chumba alimo Regina.

“Regina naamini hadi sasa umekwisha tafakari vya kutosha na uko tayari

kutueleza ukweli.” alisema Mathew.

“Tayari nimewaeleza kila kitu mlichohitaji kukifahamu. Sijawadanganya. Naomba mniamini tafadhali.” alisema Regina.

“Regina kuna kitu bado unakificha. Wewe na hao wanaojiita kamati ya Tanzania mpya mnashirikiana. Kwa nini wenzako wakataka kukuua? Aliuliza Mathew.

“Mathew nilikueleza sababu za mimi kutakiwa kuuawa.” Alijibu Regina.

“Sababu uliyotueleza bado haina uzito. Nataka utueleze ukweli kwa nini wenzako wanataka kukuua? Regina hivi sasa unasakwa na jeshi la polisi kwa tuhuma za mauaji ambayo hukuyafanya na waliokuangushia mzigo huo wa tuhuma za mauji ni hao wenzako unaoshirikiana nao. Nataka kufahamu sababu kwa nini wakufanyie haya? Lazima

ipo sababu nzito ya wewe kutakiwa kuuawa. Tueleze ukweli tafadhali.” alisema Mathew.

“Sababu kuu ya mimi kutakiwa kuuawa ni baada ya kugundulika ninamchunguza mwenyekiti. Hakuna sababu nyingine zaidi ya hiyo” alisema Regina. Mathew alimtazama kwa umakini mkubwa kwa sekunde kadhaa halafu akauliza.

“Nilikuuliza kuhusu kumpigia simu Lucy na

kumtaka amjulishe Israel Maungwana asifike msibani kwa kuwa tutakuwepo pale kumchunguza. Nauliza kwa mara nyingine tena kwa nini hukutaka tufahamu kama Israel na akina Bernadetha wanashirikiana? Mathew aliuliza. Regina aliinamisha kichwa akionekana kutafakari jambo.

“Regina hatuna muda wa kupoteza. Tafadhali tunahitaji jibu” alifoka Mathew.

“Sina jibu la kuwapa. Kila kitu nimekwisha waeleza.” alisema Regina.

“Regina huu si muda wa mzaha. Tuko katika kipindi kigumu sana tunaomba majibu tafadhali”

“Mathew nimekwisha sema sina jibu la kuwapa. Fanyeni kile mnachotaka kukifanya. I’m ready” alisema Regina. Mathew alimtazama kwa hasira.

“Regina nitakuuliza kwa mara ya mwis….” Mathew

alinyamaza baada ya Gosu Gosu kufungua mlango akaingia ndani. Mikono yake ilitapakaa damu.

“What happened? Aliuliza Mathew.

“She’s ready to talk” alijibu Gosu Gosu. Mathew alimgeukia Regina.

“Nitarudi tena kwako baada ya muda” alisema Mathew wakatoka ndani ya kile chumba huku Gosu Gosu akimkata Regina jicho kali lililobeba ujumbe wenye kutoa onyo.

Waliingia ndani ya chumba alimo Lucy. Alikuwa sakafuni akivuja damu. Lucy ambaye akina Mathew walimuacha dakika chache zilizopita si huyu waliyemkuta amelala sakafuni akilia. Sura ilibadilika. Mathew alisimama akamtazama halafu akamtaka Gosu Gosu kumketisha kitini.

“Tusipoteze muda. Nimeambiwa uko tayari kuzungumza.” Alisema Mathew. Lucy aliitika kwa kichwa.

“Good. Tuanzie katika ile picha niliyokuonesha awali. Sina haja ya kukuonesha tena kwa sababu uliitazama kwa makini tena mara mbili. Nataka uniambie unamfahamu yule mtu pichani? Aliuliza Mathew. Lucy aliitika kwa kichwa kukubali.

“Toa sauti!” alifoka Gosu Gosu huku akimsogelea. Lucy alikohoa kidogo na kusema kwa sauti ya chini.

“Ndiyo ninamfahamu.”

“Anaitwa nani? Mathew aliuliza.

“Anaitwa Regina Zanga”alijibu Lucy.

“Tumemuhoji Regina ametueleza anafanya kazi katika kampuni ya utafiti wa madini ya Tarmo. Unaifahamu kampuni hiyo? Aliuliza Mathew. Lucy ambaye bado damu iliendelea kumtoka katika majeraha aliyokuwa nayo hasa lile la chini ya jicho aliitika kwa kichwa.

“Nimekwambia tunahitaji kusikia sauti na si kuzungumza kwa ishara”alifoka Gosu Gosu na kutishia kumnasa Lucy Kofi.

“Ndiyo ninaifahamu” alijibu Lucy.

“Nataka utueleze kwa kina kuhusiana na kampuni hiyo. Nani mmiliki wake na nini hasa malengo yake?”

“Regina hakuwaeleza kuhusu kampuni hiyo? Aliuliza Lucy.

Mathew alimweleza kwa ufupi kile alichoelezwa na Regina kuhusiana na kampuni hiyo ya utafiti wa madini.

“Katika maelezo yake alituambia kuwa alitakiwa kuwasilisha taarifa zote kwako. Unaonekana ni mmoja wa watu wenye nafasi katika kampuni hiyo hivyo tunahitaji maelezo ya kina ya kuhusu hiyo kampuni” alisema Mathew. Lucy alibaki kimya akitazamana na Mathew.

“Lucy tafadhali usitupotezee muda wetu. Tunahitaji kupata maelezo tafadhali” alisema Gosu Gosu huku akiinuka na kumsogelea Lucy. Sura yake ilitisha. Lucy aliogopa.

“Nitawaeleza tafadhali naomba msiniumize” alijitetea Lucy kabla ya Gosu Gosu kumfikia.

“Hii iwe ni mara ya mwisho. Ukiulizwa kitu jibu haraka na kwa ufasaha.

Umenielewa?” aliuliza Gosu Gosu.

“Nimekuelewa”

“Good” alisema Gosu Gosu na kwenda kuketi.

“Kampuni hii ya Tarmo ilianza katika mwaka wa tatu wa awamu ya pili ya uongozi wa Rais Malaki Mnambara. Hii ni baada ya kufariki Bilionea Albert Wengela mfanyabiashara mkubwa hapa nchini. Albert ni baba wa Sophia Mnambara mke wa Rais mstaafu Malaki

Mnambara. Albert pia ni baba wa aliyekuwa waziri wa fedha wakati huo Sixmund Mnambara. Albert Wengela alifariki nchini Afrika kusini ambako aliambatana na Rais aliyefanya ziara ya siku tatu nchini humo. Rais Mnambara aliongozana na wafanya biashara zaidi ya hamsini katika ziara yake nchini Afrika kusini akiwemo Albert Wengela.” Alinyamaza akafuta damu chini ya jicho halafu akaendelea.

“Saa mbili asubuhi katika siku ya pili ya ziara ya Rais Mnambara, Bilionea Albert alikutwa amekufa ndani ya chumba cha hoteli aliyofikia jijini Johanesburg. Saa tano asubuhi siku hiyo hiyo waziri wa fedha ambaye ni mtoto wa bilionea Wengela alifariki dunia kwa ajali ya gari. Saa sita mchana iligundulika naibu waziri wa fedha naye alikutwa amefariki katika chumba cha moja ya hoteli kubwa hapa Dar es salaam. Inasemekana alifika

hotelini hapo akiwa na mwanamke ambaye hadi leo hii hajajulikana wakachukua chumba na haifahamiki mwanamke huyo aliondoka saa ngapi ila naibu waziri alikutwa amekufa. Vifo hivyo vilizua minong'ono huku wananchi na familia ya marehemu wakiitaka serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhusiana na vifo hivyo vyenye utata. Serikali iliunda timu maalum ya uchunguzi ambayo baada ya siku thelathini ilitoa majibu ya

uchunguzi wao. Katika majibu yao timu hiyo ilibainisha kuwa bilionea Wengela alifariki dunia kwa shambulio la moyo. Waziri wa fedha Sixmund Wengela inadaiwa alichanganyikiwa baada ya kupokea taarifa ya kifo cha baba yake ndiyo maana alichukua gari na kuondoka kwa kasi, alipokuwa njiani alipata ajali akafariki papo hapo. Kwa upande wa naibu waziri wa fedha inadaiwa alifariki kwa shambulio la

moyo. Taarifa hiyo ya uchunguzi haikumridhisha Sophia Mnambara mke wa Rais hivyo kumlazimu kutafuta wapelelezi kwa siri kutoka nje ya nchi ili kufanya uchunguzi. Taarifa ya uchunguzi aliyoipata ilisema kuwa vifo vile havikuwa vya kawaida. Bilionea Albert aliuawa kwa sumu na si shambulio la moyo kama ilivyodaiwa na serikali. Idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi SNSA ilitajwa kuhusika katika vifo hivyo.

Taarifa hiyo ndiyo iliyompelekea Sophia Mnambara kuanzisha kampuni ile ya utafiti wa madini kwa kumtumia mtu mwingine lakini nyuma ya pazia kampuni hiyo ikiwa na malengo mengine. Kubwa likiwa ni kuichunguza SNSA na kisha kuibomoa kabisa vile vile kuhakikisha wale wote waliohusika katika vifo vile vya baba na kaka yake wanalipa kwa kile walichokifanya. Kujibu swali lako, kampuni

hiyo ya Tarmo minerals research company ilianzishwa na Sophia Mnambara mke wa Rais kwa sababu niliyoitaja hapo juu” Lucy alinyamaza na kumtazama Mathew.

“SNSA ni idara ya siri ambayo iko chini ya Rais. Kama ilitajwa kuhusika katika mauaji hayo ya bilionea Albert lazima Rais naye anahusika katika mauaji hayo. Uchunguzi uilieleza sababu ya mauaji hayo?” Aliuliza Mathew.

“Bado uchunguzi unaendelea. Tunao watu wetu ndani ya SNSA ambao wanatusaidia katika uchunguzi huo.” Alijibu Lucy.

“Unataka kutuambia mpaka leo hii bado haijafahamika sababu ya mauaji hayo? Aliuliza Mathew.

“Ndiyo. Mpaka sasa bado uchunguzi unaendelea. Mauaji hayo japo yalifanywa na SNSA lakini yalifanywa kwa usiri mkubwa sana.” Alijibu Lucy. Mathew alimtazama kwa

sekunde chache halafu akauliza tena.

“Nataka kumfahamu Julius ni nani?

“Julius? Lucy naye aliuliza.

“Ndiyo .Umekuwa unawasiliana naye. Alikupa taarifa ya kifo cha Bernadetha, ndiye uliyewasiliana naye ukamjlisha kuwa Gavana ametoka na baadaye akakujulisha kuwa tayari wanaye Gavana. Ni nani huyu mtu? Aliuliza Mathew. Midomo ya Lucy ilicheza kama

anataka kuzungumza kitu lakini anashindwa.

“Lucy tafadhali naomba jibu. Hili si jibu la kutafuta kwani ni mtu unayemfahamu” alifoka Mathew.

“Anafanya kazi SNSA. Ni mkurugenzi wa sasa wa idara hiyo” alijibu Lucy. Ulipita ukimya mfupi halafu Mathew akauliza.

“SNSA wanahusika katika kumteka Gavana?

Lucy alishindwa kujibu akabaki kimya.

“Ulifahamu nimekutana na Gavana pamoja na Faraji Dilele nyumbani kwenu jana usiku. Faraji Dilele ameuawa tayari na anayefuatia ni Gavana. Kwa nini unataka mume wako auawe? Aliuliza Mathew. Lucy alibaki kimya.

“Una roho ya namna gani we mwanamke? Unalipwa shilingi ngapi hadi ukamuuza mumeo? Aliuliza Gosu Gosu

sura yake ikiwa imejikunja kwa hasira.

“Unafahamu kile anachokipitia Gavana hivi sasa huko katika mikono ya waliomteka? Aliuliza Ruby ambaye muda mrefu alikuwa kimya.

“Mathew naomba mnipe tena dakika tano niseme na huyu mwanamke. Ninawapenda sana wasaliti kama hawa. Ninaifahamu adhabu yao” alisema Gosu Gosu huku akisimama.

“Gosu Gosu subiri kidogo. Lucy kwa nini ukamuhukumu kifo mume wako? Amekufanyia jambo gani baya hadi ukamfanyia hivi ulivyofanya? Nijibu haraka kabla sijampa Gosu dakika anazohitaji azungumze nawe tena” alisema Mathew. Lucy alivuta pumzi ndefu na kusema.

“They’re not going to kill him.”

Kimya kilitanda.

“Baada ya Gavana kuwaeleza kile wanachokihitaji, hawatamuacha hai watamuua.” alisema Mathew.

“Hapana hawatamuua. Wamemchukua kwa ajili ya mahojiano.” Alisisitiza Lucy.

“Nini wanachokihitaji kutoka kwake? Aliuliza Mathew. Gosu Gosu ambaye bado mkono wake ulikuwa unawasha alimtazama Lucy kwa hasira.

“Wanahitaji kujua mahali mlipo”

“Kwa nini SNSA wanatutafuta? Aliuliza Mathew lakini Lucy hakujibu kitu.

“Nakuuliza Lucy kwa nini SNSA idara ya serikali wanatutafuta?

“Kwa sababu tayari mmefahamu mambo msiyopaswa kuyajua”

“Mambo gani hayo ambayo hatukupaswa kuyajua?

“Regina hajawaeleza kuhusu kile kinachoendelea? Lucy aliuliza.

“Hupaswi kuuliza swali Nyau wewe” alifoka Gosu Gosu.

“Lucy ulikuwa unawasiliana na Regina akakueleza yuko na sisi. Kwa nini ulitumia njia ndefu ya kumuuza Gavana wakati unafahamu mahali alipo Regina ndipo tulipo? Kwa nini hukuwaeleza SNSA kama unafahamu mahali tulipo? Mathew aliuliza tena.

“It’s because we have a mission.” Alisema Lucy kwa sauti ya ukali.

“Misheni ipi mliyo nayo? Mathew aliuliza.

“You won’t understand what’s going on.” alisema Lucy na kumkasirisha Mathew.

“Sipendi sana mtu anapotumia hayo maneno eti *you won’t understand*. You have to make us understand. Umenielewa Lucy?

Ulipita ukimya mfupi Lucy akionekana kuzama katika mawazo.

“Misheni ipi unayoizungumzia Lucy? Tanzania mpya? Aliuliza Mathew.

Kabla Lucy hajajibu kitu, simu ya Ruby iliita. Aliitoa mfukoni akatazama mpigaji akashituka na kumtazama Mathew.

“Kuna nini Ruby? Aliuliza Mathew.

“Gavana anapiga simu” alijibu Ruby na kumpatia Mathew simu. Sura ya Lucy ilibadilika. Aliingiwa na hofu kubwa. Mathew alitoka ndani ya kile chumba ili aipokee ile simu lakini Ruby akamzuia.

“Mathew usiipokee hiyo simu”

“Kwa nini Ruby?

“Lazima watakuwa ni watu waliomteka wanataka kufahamu mahali tulipo”

“Simu yako umeiwekea ukuta hakuna anayeweza kujua mahali ulipo.”

“Ndiyo. Hata hivyo lazima tuchukue tahadhari. Kupokea hiyo simu ni hatari sana kwa sasa” Alisema Ruby lakini tayari kidole cha Mathew kilikwisha ipokea simu.

“Gavana” alisema Mathew huku Ruby akimtazama kwa macho yaliyojaa mshangao uliochanganyika na woga.

“Mathew ! Oh ahsante Mungu.” alisema Gavana

baada ya kuisikia sauti ya Mathew.

“Mzee uko wapi? Uko salama? Aliuliza Mathew.

“Niko salama Mathew. Nimekupigia nahitaji kuonana nawe” alisema Gavana. Kilipita kimya cha sekunde chache.

“Mathew” aliita Gavana.

“Gavana uko wapi kwa sasa? Watu waliokuteka nyara wamekuachia huru? Aliuliza Mathew.

“Mathew niko huru usihofu” alijibu Gavana na kumuelekeza Mathew mahali pa kukutana kisha akakata simu.

“Anasemaje Gavana? Aliuliza Ruby.

“Jamaa waliomteka tayari wamemuachia huru”

“How? Ruby aliuliza.

“Ni kweli Mathew lazima tujiulize wamemuachiaje huru? Yawezekana ikawa ni janja yao kumtumia Gavana ili waweze

kutupata.” Aliongeza Gosu Gosu.

“Gavana anahitaji nikaonane naye.” alisema Mathew.

“Mathew huu ni mtego. Kama nilivyosema hawa jamaa wamemtumia Gavana akupigie simu wakiamini lazima utakwenda kuonana naye. Mathew sikushauri uende huko.” Alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu iwe ni mtego au si mtego lakini lazima nifike mahali hapo. Siwezi kuipuuza

nafasi hii muhimu sana” alisema Mathew.

“Mathew ninaungana na Gosu Gosu. Huu ni mtego. Ukienda hapo umekwisha. Kuna mawili aidha watakuua au watakuteka nyara. Bado tunayo kazi kubwa mbele yetu na wewe ndiye tunayekutegemea utuongoze. Please don’t go” alisema Ruby.

“Jamani msiogope. Tumekutana na hatari nyingi tumezivuka zote. Hii nayo kama ni hatari hatuna budi

kukabiliana nayo. Ni nafasi pekee ya kumuokoa Gavana kama atakuwa bado anashikiliwa mateka.” alisema Mathew na kueleza namna watakavyofanya. Gosu Gosu na Ruby walikubali mpango ule wa Mathew japo kwa shingo upande. Jackline aliitwa akaelezwa kuhusiana na mpango ule akakubali kushiriki. Bila kupoteza muda, Gosu Gosu, Ruby na Jack waliingia garini wakaondoka. Dakika mbili baadaye Mathew

naye aliondoka kuelekea mahali alikoelekezwa na Gavana. Jombaa aliachwa kuwalinda Regina na Lucy.

****

“Mlinzi ! iliita sauti ya Lucy baada ya kumuona Jombaa kupitia mlango wa kioo . Jombaa aliyekuwa nje ya kile chumba aliufungua mlango akaingia ndani.

“Unasemaje wewe mama? Aliuliza Jombaa.

“Nahitaji kwenda maliwato. Nifungue tafadhali” alisema Lucy na kumfanya Jombaa atoe kicheko.

“Hapo ulipo ndiyo choo chako. Jisaidie hapo hapo Nyau we! Alisema Jombaa.

“Tafadhali nakuomba unisaidie nimebanwa sana” aliomba Lucy.

“Nimekwambia jisaidie hapo hapo.” Alisema Jombaa na kugeuka ili atoke.

“Subiri” alisema Lucy, Jombaa akageuka.

“Unataka nini? Sipendi kupotezewa muda wangu”

“Unanifahamu mimi ni nani? Aliuliza Lucy.

“Sikufahamu lakini una sura ya kishetani.”

“Mimi ni mke wa Gavana ambaye alfajiri ya leo ametekwa. Nimewasikia hawa jamaa wakizungumza kuwa Gavana kawapigia simu. Ni kweli? Lucy aliuliza.

“Hayo mambo hayakuhusu. Tumia muda huu ulioupata kusali na kumuomba Mungu akusamehe makosa yako kwa sababu kitakachotokea watakaporejea hata shetani mwenyewe anaogopa” alisema Jombaa huku akitoa kicheko cha kejeli.

“You have to help me”

“Nilimwambia hata yule mwenzako sifahamu kiingereza hivyo unavyozungumza nami kwa kutumia lugha hiyo naona

kama unanitukana!” Alifoka Jombaa.

“Niambie unahitaji kiasi gani cha fedha nikupatie unifungue niondoke mahali hapa? Aliuliza Lucy na Jombaa akaangua kicheko.

“Sikiliza we mama. Hapa ni ukingoni mwa safari ya maisha yako. Kutoka hai humu ndani ni muujiza ambao unahitaji kumuomba Mungu aufanye. Uovu wote ambao wewe na wenzako mmeufanya zimebaki siku chache utafika mwisho.

Jiandae” alisema Jombaa na kuufunga mlango akatoka akamuacha Lcy akitukana matusi makubwa ya nguoni. .

****

Gari la akina Gosu Gosu lilifika katika ile baa ambayo Gavana alimtaka Mathew wakutane. Baada ya kuegeshwa Jackline alishuka garini na kwenda kujibanza mahali

ambako aliweza kuona kwa uzuri kila kilichokuwa kinaendelea kule katika maegesho ya magari. Alimpigia simu Mathew aliyekuwa anatumia simu ya Ruby akamjulisha kuwa tayari wamefika pale katika ile baa na haoni tatizo lolote. Mathew aliwataka waendelee kuwa makini kuchunguza kila kinachoendelea mahali pale.

Dakika saba tangu akina Gosu Gosu wafike mahali pale, gari la Mathew nalo liliingia

taratibu na kuelekea moja kwa moja maegesho. Jicho lake lilizunguka kama Kinyonga kuchunguza kama kuna hatari yoyote. Baada ya kuegesha alichukua simu akampigia Gavana na kumjulisha kuwa tayari amefika mahali pale. Gavana alimwelekeza gari alimo.

“Unaweza kutoka nje tafadhali ili nihakikishe kweli uko mahali hapa? Aliuliza Mathew.

“Nchi nzima wanafahamu nimetekwa. Nikionekana mahali hapa kila kitu kitaharibika ndiyo maana nimejificha ndani ya hili gari sitaki watu wanione. Hakuna tatizo Mathew naomba uniamini” alisema Gavana. Mathew alimpigia Jack simu akamjulisha kuwa anashuka garini ili wawe makini. Aliufungua mlango wa gari taratibu akashuka na kuanza kupiga hatua kuelekea katika gari alimo Gavana. Gosu Gosu,

Ruby na Jack wote walikuwa wanamfutilia Mathew. Kila mmoja alikuwa tayari muda wowote kama kungetokea hatari.

Mathew alilikaribia gari aliloelekezwa na Gavana, mara taa za mbele ziliwaka mara mbili haraka haraka kumpa ishara Mathew kuwa ni katika gari lile. Alilisogelea kwa tahadhari kubwa huku akiangaza kila upande, mara kioo kilishushwa. Mkono wa Mathew ulikuwa mwepesi

mno. Mara tu kioo kiliposhushwa tayari mkono wake wa kulia ulikwisha ifikia bastola akaitoa na kuielekeza dirishani.

"Mathew it's me." ilisema sauti ambayo Mathew aliitambua ni sauti ya Gavana. Bado bastola ikiwa mkononi alilisogelea gari. Gavana alivua kofia na miwani aliyokuwa amevaa ili kuzuia asitambulike, taa ya ndani ya gari iliwashwa na Mathew akamtambua. Macho ya Mathew yalitua kwa

mtu aliyekuwa pembeni ya Gavana akiwa mtupu hana nguo hata moja.

“Mathew get in the car” alielekeza Gavana na Mathew akafungua mlango akaingia garini.

“Mzee uko salama? Nini kinaendelea hapa? Huyu mtu ni nani? Aliuliza Mathew.

“Mathew usihofu niko salama kabisa.”

“Huyu ni nani? Kwa nini hana nguo? Aliuliza Mathew.

“Huyu ndiye aliyeniokoa. Anahitaji kuzungumza nawe”

“Who are you? Aliuliza Mathew.

“Naitwa Julius Mukoke. Ni mkurugenzi wa SNSA.”

“Julius? Mathew alishangaa.

“Ndiyo.”

“Mathew tafadhali mimi si mtu hatari kwako. Nimemuokoa Gavana ili anisaidia niweze kuonana nawe. Nina jambo la muhimu

sana la kukwambia. Naomba unipe nafasi ya kuzungumza nawe nikueleze kile nilichonacho” alisema Julius. Mathew alimgeukia Gavana.

“Mathew usiwe na hofu naye. Nimekwisha chukua tahadhari zote nimemkagua kama ana kifaa chochote mwilini sijamkuta na kifaa chochote. Ili kujiridhisha zaidi nimemvua mavazi yake nikayatupa ndiyo maana unamuona mtupu. Naomba

umsikilize tafadhali.” alisema Gavana.

“Gavana ninataka neno lako la mwisho la kunihakikishia kuwa huyu mtu ni salama na hatuingizi katika mtego.” alisema Mathew.

“Mathew ninafahamu kazi kubwa unayoifanya hivyo niko tayari kuutoa uhai wangu kuliko kuhatarisha uhai wako. Niam……” Kabla Gavana hajamaliza, Mathew alimtandika Julius pigo moja

mahali ambapo palimpoteza fahamu.

“Mathew niamini tafadhali huyu mtu hana hatari yoyote kwetu.” alisema Gavana akionekana kushangazwa na kitendo kile alichokifanya Mathew.

“Hawa watu si wa kuwaamini hata kidogo” alisema Mathew huku akimvuta Julius akamtoa katika kiti cha dereva akamrudisha katika kiti cha nyuma. Alimpigia simu Jack

akamtaka aendeshe gari lake waondoke mahali pale. Alikaa katika kiti cha dereva akawasha gari na kuondoka.

“Unaendeleaje Gavana?” Aliuliza Mathew baada ya kutoka katika ile baa.

“Nimefurahi kukuona tena Mathew Mulumbi. Sikutegemea kabisa”

“Nini kilitokea wale jamaa walipokuteka nyara? Aliuliza Mathew.

Gavana alivuta pumzi ndefu akarudisha picha ya tukio lile namna lilivyotokea akageuka akamtazama Julius aliyekuwa amelala hana fahamu halafu akasema.

“Hawa watu ni wakatili sana.” Alimueleza Mathew namna alivyotekwa alfajiri wakati akielekea kanisani. Alieleza mateso aliyopitia tangu alipotekwa.

“Ni mateso makali kwa mtu wa umri wangu lakini nilivumilia. Nilikuwa tayari

kupoteza uhai wangu kuliko kukubali ninakufahamu” alisema Gavana akaendelea kumweleza Mathew namna wale jamaa walivyomrubuni mke wake akaeleza ukweli wote kuhusu kukutana kwao. Alimweleza Mathew namna alivyowadanganya kuwa ana miadi ya kukutana naye usiku ule hadi alivyochukuliwa na Julius.

“Pole sana mzee wangu kwa yote uliyoyapitia. Ni mambo magumu sana. Ahsante kwa

kuvumilia mateso na kufumba mdomo wako kutokusema chochote kuhusu mimi. Pamoja na hayo nataka kukujulisha kuwa Faraji Dilele ameuawa.”

“Ameuawa?” Gavana alishangaa.

“Ndiyo ameuawa.” Mathew alimweleza kila kitu kilichotokea kuanzia walivyomuokoa Faraji asubuhi hadi alivyompeleka kwa mwanaye.

“Nimeshituka sana. Mungu amrehemu. Alikuwa rafiki yangu mkubwa.”

“Walio muua naamini ni hawa hawa waliokuteka nyara. Ni watu wabaya sana hawa” alisema Mathew. Alimweleza pia Gavana kuhusiana na Regina.

“Mathew nilikupa angalizo toka awali kuwa mwanamke yule ni hatari sana. Ni yeye aliyewapa hawa washenzi habari zetu.”

“Mzee suala hili ni pana zaidi ya tulivyodhani. Tutazungumza kila kitu tukifika katika maficho yetu ya muda. Kwa sasa kuna kitu nataka kufanya” alisema na kupunguza mwendo wa gari akalisimamisha kandoni mwa barabara. Akina Gosu Gosu waliokuwa wanalifuata kwa nyuma gari lile nao walisimama. Mathew alishuka garini akamtaka Gavana ashuke akaingia katika gari la nyuma. Akisaidiana na Gosu

Gosu walimshusha Julius wakamuingiza katika gari lingine. Gari lile la Julius liliachwa pale kandoni mwa barabara.

“Lazima tuchukue tahadhari kwa sababu magari ya SNSA yana vifaa vya kuyafuatilia na kujua mahali yalipo” alisema Mathew na safari ikaendelea.

****

Julius alishushwa garini baada ya kufika katika maficho ya akina Mathew akaingizwa ndani.

“Ninawashukuru sana vijana kwa jitihada zenu. Nawaomba msikate tamaa endeleeni kupambana. Watu hawa ni hatari na mipango yao kwa nchi yetu ni mibaya sana” alisema Gavana akiwa

amejipumzisha sofani. Kwa mara ya pili aliwaeleza kwa kifupi kile kilichomtokea baada ya kutekwa nyara alfajiri.

“Ni kwa sababu ya juhudi zenu ndiyo maana waliniteka nayara ili wafahamu mahali mlipo. Tayari wameingiwa hofu kwa hatua ambazo mmezipiga hadi sasa. Narudia kuwaomba msikate tamaa japo mapambano ni magumu kwani hawa jamaa ni mtandao mpana wenye nguvu kubwa.” Alisema Gavana.

Mathew aliitumia nafasi ile kumweleza tena kila kitu kilichotokea kwa siku nzima hadi walivyofanikiwa kugundua Regina alikuwa na simu ambayo aliitumia kwa mawasiliano.

“Mathew mwanamke yule ni Nyoka mwenye sumu kali ndiyo maana nilikuonya tangu awali uwe makini naye sana. Nina uhakika kuna mambo anayafahamu kuhusu mwanangu Kelvin ndiyo maana nimekuwa nikiweka

wapelelezi kumchunguza ili niupate ukweli. Kwa bahati mbaya wapelelezi wote wamekuwa wakiuawa kabla hawajafanikisha uchunguzi wao. Ni wewe pekee uliyepiga hatua na kugundua kuwa Kelvin alikuwa mpelelezi wa siri wa SNSA. Imekuwa vyema mmemgundua mapema vinginevyo nyote mngeuawa kwani angewajulisha wenzake kila mnachokifanya.” alisema Gavana.

“Gavana kuna jambo nataka kukujulisha. Ni jambo zito lakini naomba ulipokee kwani lazima ulifahamu” alisema Mathew.

“Ni jambo gani hilo? Ni kuhusiana na mwanangu Kelvin? Aliuliza Gavana.

“Hapana halihusiani na Kelvin” alisema Mathew na kumtazama Gavana. Alionekana kutafuta sehemu ya kuanzia.

“Mathew naomba nieleze tafadhali.”

“Baada ya kuichunguza simu ya Regina, tumegundua alikuwa akiwasiliana na namba moja tu ambayo tulipoichunguza tukagundua ni namba ya mke wako Lucy” alisema Mathew. Kimya kilitawala mle ndani. Gavana aliwatazama akina Mathew kwa zamu.

“Mathew tafadhali naomba uniambie hicho ulichoniambia si kitu cha kweli.”

“Mzee ni kweli kabisa. Tumechunguza tukajiridhisha

namba iliyowasiliana na Regina ni ya mkeo Lucy.”

“That’s impossible!” Alihamaki Gavana.

“Mzee ni ukweli mtupu.” alisema Mathew na kumpa Gavana nakala ngumu ya mawasiliano yote ya Regina na Lucy. Mara Ghafla Gavana alianguka na kupotea fahamu. Lilianza zoezi la kumsadia Gavana arejewe na fahamu.

“Hili ni jambo zito sana ndiyo maana huyu mzee ameshituka hadi akapoteza

fahamu. Inaumiza unapogunda mtu aliyeapa mbele ya madhabahu atakuwa nawe katika shida na raha, mvua na jua amefanya kitendo kama alichokifanya Lucy.”alisema Mathew.

“Inaumiza sana unapogundua miaka yote umelala kitanda kimoja na Nyoka. Watu wa aina hii adhabu yao ni kuwatoboa macho na kuwakata ulimi washindwe kuona wala

kuzungumza” alisema Gou Gosu akiwa na hasira kali.

****

“Pole sana mzee” alisema Mathew baada ya Gavana kurejewa na fahamu.

“Mathew natamani wale jamaa SNSA wangeniua ili nisiufahamu ukweli huu mchungu. Nimeumia sana.” alisema Gavana.

“Mzee, utatusamehe lakini ni wajibu wetu kukueleza ukweli” alisema Mathew.

“Mathew hamjafanya vibaya. Ninawashukuru sana kwa kunieleza ukweli. Hata hivyo bado ninahitaji maelezo zaidi ili nielewe kiundani jambo hili.” Alisema Gavana.

“Kama nilivyokueleza mzee kuwa baada ya kuichunguza simu ya Regina tuligundua alikuwa anawasiliana na namba ya mkeo. Tulifanya utaratibu tukaipata simu ya mke wako tukaifanyia uchunguzi ndipo tukapata hiki ulichokiona katika hii nakala ngumu.”

“Mliipata simu yake, yeye mkamuacha?” Aliuliza Gavana.

“Hapana hatukumuacha, tumemchukua tunaye hapa tunaendelea kumuhoji”

alisema Mathew na kumfanya Gavana ashushe pumzi.

“Nahitaji kuonana naye ana kwa ana.” alisema Gavana huku akisimama.

“Utaonana naye lakini kabla ya kuonana naye unapaswa kulifahamu jambo hili kwa undani.” Alisema Mathew na Gavana akaketi.

“Alfajiri mkeo alitumiwa ujumbe na Julius kuhusu kifo cha Bernadetha. Dakika chache baada ya kuupokea ujumbe

huo mkeo alimpigia Julius simu”

“Ilikuwa saa ngapi? Aliuliza Gavana na Mathew akamjulisha Gavana muda ambao Julius alituma ujumbe.

“Muda huo nilikuwa bado katika ibada. Nina kawaida ya kuamka saa tisa usiku na kufanya ibada hadi saa kumi na moja na nusu ambapo hujiandaa kwenda kanisani kuhudhuria misa ya asubuhi kanisani” alisema Gavana.

“Ujumbe mwingine kwenda kwa Julius ulikuwa mfupi tu *he’s on move*. Tunahisi ujumbe huu alikuwa anamjulisha Julius kuwa umeondoka nyumbani. Baada ya muda mfupi uliingia ujumbe mwingine kutoka kwa Julius ukimjulisha Lucy *we have him*. Hapa tayari ulikuwa umetekwa”

Gavana jasho lilimtoka.

“Ee Mungu nipe nguvu ya kulibeba jambo hili. Ni zito kwangu.” Alisema Gavana.

“Kwa ujumbe huo ambao Lucy na Julius walitumiana haina shaka hata kidogo kuwa mke wako alishiriki katika mpango wa kukuteka nyara.”

“Hilo linaniumiza mno. Lucy ni mke wangu ambaye nimeishi naye kwa zaidi ya miaka thelathini sasa kwa nini anifanyie haya? Kwa nini anitoe nikauawe? Aliuliza Gavana.

“Baada ya kumuhoji Regina ametueleza mambo mengi kuhusu yeye” Mathew

alimweleza kila kitu kuhusiana na kile alichoelezwa na Regina kuhusu kampuni ya utafiti wa madini.

“Mathew unazidi kunichanganya. Una maanisha mke wangu naye yumo katika kampuni hiyo ya kijasusi? Je naye ni jasusi? aliuliza Gavana.

“Bado hatujafahamu kama ni mpelelezi. Tutafahamu mambo mengi zaidi kuhusiana naye kadiri tunavyoendelea kumuhoji” alisema Mathew.

“Mathew, siwafichi vijana wangu haya mnayoniambia yameniogopesha mno. Nimemuogopa mke wangu.”

“Mzee haya tunayokwambia ni mambo ya kweli kabisa. Tukiachana na hayo ya kampuni, tunahisi Lucy pia ni mshirika wa wanaojiita kamati kuu ya Tanzania mpya lakini tufahamu zaidi pale tutakapoendelea kumuhoji. Imekuwa vyema Julius naye yuko hapa kwani wote hawa watatu ni mtandao mmoja.

Regina amedai yeye huwasilisha taarifa kwa Lucy ambaye naye huziwasilisha kwa Julius. Bado kuna mkanganyiko hapa tunahitaji kufahamu kile kinachoendelea.” alisema Mathew.

“Nadhani tutapata majibu mazuri kutoka kwa Julius. Amekiri yuko tayari kuwaeleza kila kitu kinachoendelea kwa kuwa tayari amegeukwa na wenzake wanataka kumuua. Sehemu pekee salama kwake

kwa sasa ni hapa kwenu. Ana mambo mengi ambayo atawaeleza na ameahidi kunipa ukweli wote kuhusiana na suala la Kelvin” alisema Gavana.

“Hakuna kupoteza muda. Ni wakati wa kuufahamu ukweli kutoka kwa Julius” alisema Mathew.

“Mathew kabla ya zoezi hilo naomba tafadhali unipeleke nikamuone yule mke wangu japo kwa dakika chache” aliomba Gavana. Mathew

alimtaka amfuate. Walielekea katika chumba alimo Lucy. Aliufungua mlango akaingia ndani na nyuma yake alifuata Gavana. Lucy alipatwa na mshituko alipomuona mume wake akapoteza fahamu.

“Nadhani tutalazimika kuwa na daktari usiku huu kwa sababu ya hii mishituko wanayoipata hawa watu.” aliwaza Mathew na kutoa maelekezo kwa Jack kumsaidia Lucy. Pamoja na utu uzima wake lakini Gavana alishindwa

kuyazuia machozi kumtoka. Mathew alimtaka watoke mle ndani wakarejea katika chumba cha awali na Gosu Gosu akatumwa kwenda kumchukua Julius ambaye tayari alikwisha rejewa na fahamu. Aliingizwa ndani ya kile chumba walimokuwamo akina Mathew.

“Hallo Julius. Karibu sana mahali hapa.”

“Ahsante” alijibu Julius.

“Jina langu ni Mathew Mulumbi. Sina haja ya

kujieleza zaidi kwa kuwa naamini unanifahamu, taarifa zangu zote wewe na wenzako mnazo. Wenzangu hapa ni Gavana wa benki kuu. Mwingine ni Papi Gosu Gosu. Huyu ni mwanajeshi ambaye naamini naye tayari unamfahamu. Wa mwisho niliyenaye humu ni Ruby.” Alisema Mathew.

“Nimefurahi kukutana nanyi na kuwafahamu ndugu zangu.” Alisema Julius.

“Sisi siyo ndugu zako.” Alisema Gosu Gosu.

“Julius uko hapa kwa maombi maalum kutoka kwa mzee wetu Gavana ambaye ameomba tukusikilize una jambo la muhimu la kutueleza. Kabla ya kutueleza chochote kuna maswali machache ambayo nataka kukuuliza”

“Uliza chochote nitakujibu” alisema Julius. Mathew aliichukua simu ya Ruby akafungua sehemu ya

kuhifadhi picha akamsogelea Julius.

“Nataka ukiri kama unawafahamu watu ambao nitakuonesha picha zao” alisema Mathew na kumuonesha Julius picha ya Lucy.

“Huyu ninamfahamu. Ni mke wa Gavana”

“Good” alisema Mathew na kufungua picha nyingine.

“Huyu naye ninamfahamu. Anaitwa Regina Zanga” alisema Julius.

“Ahsante sana kwa kukubali kuwa unawafahamu. Hawa wote wawili tunao hapa kwa mahojiano”

“Mnao hapa? Alishangaa Julius. ,

“Ndiyo. Tunao hapa. Bado tunaendelea kuwahoji. Nimeanza na utangulizi huo ili kukupa angalizo kuwa usithubutu kutueleza uongo wowote kwani mambo mengi

tayari tunayafahamu. Karibu tupe maelezo yako” alisema Mathew. Julius alikohoa kidogo kuweka sawa koo lake halafu akasema.

“Jina langu ni Julius Mukoke. Ni mkurugenzi oh sorry nilikuwa mkurugenzi wa idara ya siri ya usalama wa nchi kifupi SNSA.”

“Unasema ulikuwa mkurugenzi wa SNSA, kwa sasa wewe si mkurugenzi? Aliuliza Gosu Gosu.

“Nilikuwa mkurugenzi hadi giza lilipoingia lakini muda huu ninapozungumza nanyi mimi si mkurugenzi tena. Hapa mnazungumza na Julius Mukoke kama nilivyojitamblisha kwenu”

“Endelea” alisema Mathew.

“SNSA ni idara ya siri ya serikali ambayo iko chini ya ofisi ya Rais”

“Tunafahamu kuhusu SNSA. Tuendelee na mambo mengine” alisema Mathew.

“Yawezekana mnaifahamu kwa kuisikia au kwa kuelezwa kifupi. Naomba mnipe nafasi niwaeleze kuhusu idara hii na mambo yanayofanywa na idara hii kwa siri.” Alisema Julius.

“Go ahead” alisema Mathew.

“SNSA ni idara iliyo chini ya Rais mwenyewe. Viongozi wake wanawajibika kwa Rais moja kwa moja bila kupitia kwa mtu mwingine yeyote. Kama lilivyo jina lake hata mambo yake yote yanafanyika

kwa siri kubwa. Ni idara yenye mtandao mpana na uwezo mkubwa wa kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa bila kutegemea idara nyingine yoyote ya serikali. SNSA wana kila kitu kinachohitajika katika idara ya usalama. Wanatumia teknolojia ya kisasa kabisa, wameunganishwa kwa siri na mifumo ya idara na taasisi zote za serikali, mitandao ya simu, kamera zote za barabarani n.k. Kwa ujumla ni idara yenye uwezo mkubwa sana kubaini

hatari yoyote ndani ya nchi na kuiondoa mara moja bila idara nyingine za usalama kuhusishwa. Fungu la kuendesha idara hiyo ni Rais anayefahamu linakotoka. Sisi tunawasilisha bajeti yetu kwake. Hakuna wakati tumewahi kukwama kitu chochote kile.” Alinyamaza akameza mate akaendelea.

“Kutokana na uwezo na usiri wake, idara hii imekuwa ikitumiwa kama chombo binafsi cha Rais kwa kuwa

ndiye kiongozi wake mkuu. Imekuwa ikitumiwa kuwanyamazisha wapinzani wa serikali na wale wote ambao wanaonekana kuwa kikwazo kwa Rais kuongoza. Zimewahi kutokea ajali mbali mbali za viongozi zilizopelekea vifo vyao. Wakati mwingine kumetokea vifo vya ghafla vya viongozi. Kwa asilimia kubwa SNSA wanahusika katika ajali na vifo hivyo. Tunafanya hivyo kwa maelekezo ya mkubwa wetu ambaye ni Rais. Nikipata

nafasi huko mbele nitawaeleza mauaji yote ambayo SNSA imeshiriki.” Alinyamaza akawatazama akina Mathew waliokuwa wanamsikiliza kwa makini sana.

“SNSA ilianza kutumiwa kisiasa na Rais Malaki Mnambara pale alipotaka kusambaratisha upinzani hapa nchini. Tulipachika watu wetu ndani ya vyama avya siasa tukazidaka siri zao zote na namna wanavyoendesha vyama vyao na baada ya hapo

kilianzishwa chama cha ukombozi. Hiki kilikuwa na nguvu kubwa iliyopelekea vyama vya upinzani nchini kuanza kupoteza uelekeo na vingine kufa kabisa. Mgogoro uliibuka ndani ya chama kinachotawala baada ya Rais Mnambara kutaka kubadili katiba ili atawale kwa kipindi kingine cha tatu. Jambo hilo halikupokelewa vyema katika chama chake hivyo hoja hiyo haikuungwa mkono. Jambo

hil…….” Julius alikatishwa na Mathew.

“Tayari tunafahamu kuhusu jambo hilo pia”

“Please let me finish” aliomba Julius.

“ Go ahead” alisema Mathew na Julius akaendelea.

“Kutokuungwa mkono kwa hoja yake ya kubadili katiba ili atawale kwa kipindi kingine cha tatu kulimuudhi sana Rais Malaki. Aliazimia kukiondoa madarakani chama chake

ambacho bado kinatawala hadi sasa. Ni hapo ndipo kilipoibuka chama cha ukombozi wa Afrika kikawa na nguvu kubwa na kukibomoa chama cha Ukombozi."

"Nataka kufahamu je chama hiki cha ukombozi wa Afrika kilianzishwa na Rais Mnambara? Aliuliza Mathew.

"Ni kweli. Chama cha ukombozi wa Afrika kilianzishwa kwa malengo ya kukiondoa madarakani chama kinachotawala. Japo haitajwi

lakini ni kweli Rais Mstaafu Malaki Mnambara ndiye aliyekiasisi chama kwa siri chama cha ukombozi wa Afrika. Hata baada ya kuondoka madarakani lakini bado Malaki Mnambara ana uchu wa madaraka. Naweza kusema bado Mnambara anaongoza nchi hii. Rais aliyeko madarakani sasa amekuwa akiongoza kwa maelekezo ya Malaki Mnambara" alinyamaza Julius

baada ya Mathew kuonesha kutaka kuuliza jambo.

“Julius hebu twende taratibu. Unatuchanganya unaposema kuwa Rais mstaafu Malaki Mnambara bado anaendelea kuongoza nchi hii kupitia Rais wa sasa na lengo lake lingine likiwa ni kukiondoa madarakani chama kinachotawala. Tunavyofahamu Rais mstaafu Malaki Mnambara tayari amefariki dunia.”

“That’ s a big lie.” Alisema Julius.

“Huo ni uongo wa mchana. Malaki Mnambara hajafa kama inavyodaiwa. Yupo hai. Kifo chake kilitengenezwa ili kumaliza kile kilichoelezwa kuwa mashambulizi makali dhidi yake kutoka ndani ya chama chake kinachotawala. Baada ya tetesi kuibuka kuwa Malaki ndiye aliyeasisi chama cha ukombozi wa Afrika, chama chake kiliingiwa na hofu yawezekana lengo lake ni

kukiondoa madarakni chama hicho hivyo ilianza mipango ya kummaliza kabisa kisiasa ili asiweze kufikia malengo yake. Hapo ndipo zilipoanza kuibuka tuhuma mbali mbali za ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka yakimuhusisha Rais Mnambara alipokuwa madarakani. Zilifunguliwa kesi zaidi ya saba mahakamani. Kama kesi hizo zingeendelea basi zingemfikisha pabaya Malaki Mnambara hivyo kikatengenezwa kifo chake.

Alipata kibali cha kwenda nje ya nchi kwa matibabu na akiwa huko ilitanganzwa amefariki dunia. Ukweli ni kwamba Malaki Mnambara yuko hai.” Alisema Julius.

“Julius una uhakika na hicho unachotuambia? Mathew aliuliza.

“Nina uhakika mkubwa. Malaki Mnambara yuko hai. Ni watu wachache sana ambao wanafahamu siri hii”

“Kama yuko hai yuko nchi gani? aliuliza Gosu Gosu.

“Sifahamu yuko nchi gani kwani inafichwa kwa ajili ya usalama wake lakini yuko hai” alijibu Julius.

“Julius, hiki unachokisema ni kitu kikubwa sana ambacho kama kikiwekwa wazi kitaisimamisha dunia kwa muda. Dunia nzima wanafahamu Malaki alifariki dunia.” alisema Gavana.

“Naomba msiwe na shaka nami hata kidogo. Nina uhakika huo kuwa Malaki hajafariki dunia. Ni mzima wa

afya tele na anaendelea na maisha yake ya starehe kama kawaida”

“Malaki hawezi kutengeneza jambo hili peke yake. Lazima wapo waliomsaidia. Aidha nchi Fulani au chama Fulani.”alisema Mathew.

“Ni kweli unachokisema Mathew Mulumbi. Tangu alipoingia madarakani Malaki Mnambara amekuwa ni kibaraka wa mabeberu. Nitaeleza baadaye jambo hilo

lakini kwa sasa naomba nijielekeze zaidi katika mipango yake dhidi ya nchi hii” alisema Julius.

“Endelea tunakusikiliza” alisema Mathew.

“Kama nilivyoeleza awali kuwa Malaki Mnambara malengo yake makubwa ni kukiondoa madarakani chama kinachotawala sasa na kukiweka chama alichokiasisi cha ukombozi wa Afrika. Katika mpango huu hayuko peke yake. Anasaidiwa na nchi

moja kubwa ambayo malengo yake ni kuchuma utajiri mkubwa ulioko hapa Tanzania. Ili kufanikisha mpango huo imetengenezwa kamati inaitwa *Kamati kuu ya Tanzania mpya*. Hii ndiyo inayoratibu mpango mzima wa kukiondoa madarakni chama kinachotawala na kukiingiza chama cha ukombozi wa Afrika. Kamati hii inaundwa na watu wazito. Wamo matajiri wakubwa, wamo pia viongozi serikalini. Mimi pia nilikuwa

mmoja wao kama mkuu wa SNSA ambayo imekabidhiwa majukumu ya kushughulikia masuala yote ya usalama wa mpango huo.”

“Unaweza ukatueleza nani na nani wamo katika kamati hiyo? Aliuliza Gavana.

“Nitawaeleza lakini fahamuni ni watu wazito wenye nguvu. Karibu kila idara nyeti katika nchi hii imeshirikishwa katika mpango huo. Wapo pia viongozi wengine ambao wako nje ya

kamati hiyo inayoratibu mpango wa Tanzania mpya na mmoja wao ni Rais wa sasa Dkt Nehemia Nchelela. Niliwaeleza awali kuwa Dkt Nehemia ni kama picha tu ya Rais lakini mambo mengi yanafanywa na Malaki Mnambara.Wako kundi moja. Wanataka kukiondoa madarakani chama kinachotawala na kuweka mtu wao kwa faida ya mabeberu. Nilisema kuwa jambo hili linafadhiliwa na nchi moja

kubwa hivyo wote wanaohusika katika kulifanikisha wameahidiwa fedha nyingi mno. Ni fedha nyingi ambazo hawawezi kuzipata hata kama wakifanya kazi kwa maisha yao yote.Hiyo ni sababu kmati hiyo haitaki kutokee jambo lolote la kuwakwamisha ndiyo maana hata SNSA imebadilishwa malengo yake na kuwa sehemu ya kufanikisha mpango huo.” Alinyamaza tena kidogo.

“Ni namna gani wanapanga kukiondoa madarakani chama kinachotawala ambacho kina mtandao mpana nchi nzima na mamilioni ya wafuasi? Aliuliza Mathew.

“Nilisema kuwa kila idara nyeti ambayo wanadhani inaweza kuwa na umuhimu katika kufanikisha mpango huo imejumuishwa katika hiyo kamati kuu. Tume ya taifa ya uchaguzi ni wadau pia wa mpango uo. Mtaona ni namna gani hawa watu walivyojiandaa

kwa kila namna kuhakikiha wanafanikisha mipango yao. Hawataki kusikia kitu kushindwa. Wana uhakika kwa asilimia kubwa lazima wafanikishe mpango wao” alisema Julius.

“Dah !” aliguna Gavana.

“Kama hadi tume ya uchaguzi wamo katika mpango huu basi ngoma ni nzito hii” aliongeza Gosu Gosu.

“Endelea Julius. Kuna mengi tunahitaji kuyafahamu bado” alisema Mathew.

“Kila kitu kilikwenda vizuri na hakukuwahi kutokea mkwamo wowote hadi pale yalipofanyika maamuzi ya kumuua Regina Zanga”

“Nini hasa sababu ya kutaka kumuua Regina.? Aliuliza Mathew.

“Nitalieleza hilo huko mbele lakini kwa ufupi Regina alitaka kuharibu mambo ndiyo maana ikaamriwa auawe. Kilichotokea Arusha nyote mnakifahamu. Matatizo yote yalianzia hapo baada ya

Mathew Mulumbi kuingia mchezoni. Jina lako lilipotua katika meza ya *kamati kuu ya Tanzania mpya* ilitanda hofu kubwa. Zilifanyika juhudi kubwa za kuhakikisha wewe na wenzako wote mnapatikana kwa haraka lakini juhudi hizo ndizo zimezua mvurugano mkubwa uliopelekea hata kusalitiana na kuanza kuuana wenyewe kwa wenyewe."

"Julius kabla hujaendelea nataka kufahamu jambo. SNSA mlibeba majukumu yote ya

kiusalama katika mpango huu. Kwa nini hamkumuua Regina hadi mkamtumia mtu mwingine kufanya mauaji hayo?” Mathew aliuliza.

“Niliwafahamisha hapo awali kuwa huu si mpango wa Malaki Mnambara bali ni mpango wa nchi kubwa zinazoumezea mate utajiri mkubwa wa Tanzania na Afrika kwa ujumla. Umetengenezwa mpango ambao utahakikisha vibaraka wa mabeberu hao wanaingia madarakani.

Mpango huo umezilenga nchi kumi zenye utajiri mkubwa wa rasilimali mbali mbali. Tanzania na Congo zimo katika mpango huo. Wakati Tanzania kuna mpango wa Tanzania mpya, nchini Congo nako kuna mpango wa Congo mpya. Kwa maelekezo ya wakubwa hao,wametutaka tushirikiane na wenzetu wa Congo mpya na kuwasaidia. Wenzetu mpango wao ni tofauti na wa kwetu. Mpango wao wa Congo mpya

wanautengeneza nje ya Congo wakati sisi tuna……”

“Tayari tunafahamu jambo hilo. Nataka utueleze sababu kwa nini akatumika Gosu Gosu kufanya mauaji na si SNSA? Mathew aliuliza.

“Ni makubaliano ya kamati kuu. Waliamua kumtumia raia wa Congo ambaye ili hata kama mambo yangeharibika ingekuwa rahisi kumtorosha nchini Tanzania na kumpeleka Congo.”

“Kwa nini ilichukua muda mrefu kuandaa mauaji hayo? Gosu Gosu aliuliza.

“Ni kwa sababu bado Regina alikuwa anachunguzwa kufahamu nyendo zake na watu anaoshirikiana nao”

“Waligundulika watu anaoshirikiana nao?

“Mtu pekee aliyafahamika ni Amani ambaye alikuwa dereva wa mwenyekiti wa chama cha ukombozi wa Afrika.”

“Sikiliza Julius hayo yote unayotueleza tunayafahamu. Tunachotaka kukifahamu sisi ni sababu ya Regina kutakiwa kuuawa. Kwa ufupi tu ni kwamba, baada ya kumuokoa Regina kule Arusha tulimuuliza kama anawafahamu wanaotaka kumuua na moja kwa moja alikitaja chama chake kuwa ndio wanaotaka kumuua. Sababu ya kutakiwa kuuawa ni kutokana na kugundua baadhi ya siri zao na hasa huu mpango

wa Tanzania mpya. Baadaye tukagundua tena kuwa Regina alikuwa ni mmoja wa washiriki wa mpango huo wa Tanzania mpya. Hapo ndipo panapotuchanganya na hata Regina mwenyewe ameshindwa kutupa jibu, kwa nini auawe na wenzake wanaoshirikiana katika misheni moja? Jibu mnalolitoa hapa ni kuwa alikuwa anamchunguza mwenyekiti wa chama chake cha ukombozi wa Afrika. Kwa nini amchunguze

Israel Maungwana wakati wote wanashiriki katika misheni moja ya Tanzania mpya? Kuna kitu bado kinaelea kuhusu jambo hili ambacho nahitaji kukifahamu. Sitaki unipe sababu nyepesi kama hiyo ya kumchunguza Israel.” Alisema Mathew. Kilipita kimya mle ndani.

“Julius kama umekuja hapa kutueleza ukweli naomba usifiche kitu chochote. Najua kuna kitu unakifahamu kuhusu Regina kutakiwa kuuawa lakini

unaogopa kukisema. Tafadhali naomba majibu. Hii ni nafasi pekee umeipata itumie vyema” alisema Mathew.

“Kwa kuwa nimeamua kuungana nanyi sina sababu ya kuwaficha chochote.” alisema Julius.

“Bado hatujakukubali kujiunga nasi hivyo usizugumze kama vile tayari wewe ni mwenzetu”alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu yuko sahihi, kuingia kwako katika timu yetu

kutategemea na yale utakayotueleza kama yana manufaa kwetu. Acha kupoteza muda na utueleze mambo ya msingi ya kutushawishi tukukubali kama mwenzetu" alisema Mathew.

"Kwanza kabisa Regina hajawahi kuwa mshirika wa mpango wa Tanzania mpya." Kauli ile iliwashangaza akina Mathew.

"Kwa mdomo wake, Regina alikiri kuwa mshirika wa mpango huo wa Tanzania

mpya. Iweje useme hakuwa muhusika?” aliuliza Mathew.

“Mathew kuna mambo mengi ambayo hamjaelezwa ukweli. Mimi niko hapa ili kuwapeni ukweli. Regina hakuwa mshiriki wa mpango huo wa Tanzania mpya. Mtu pekee ambaye anashiriki mpango huo kutoka chama cha ukombozi wa Afrika ni mwenyekiti wao Israel Maungwana ambaye naye ni miongoni mwa wale washiriki ambao wanaitwa washiriki wa

gizani yaani wako nje ya kamati. Hao ni wachache sana akiwemo pia Rais Dkt Nehemia. Chama kimepewa majukumu ya kuhakikisha kinashiriki uchaguzi mkuu. Hata ndani ya chama hicho cha ukombozi wa Afrika mpango huu wa Tanzania mpya haujulikani. Anayeufahamu ni mwenyekiti pekee. Mpango huu unaendeshwa kwa siri kubwa sana hivyo mtu mdogo kama Regina hawezi kushirikishwa. Regina kama

ilivyo kwa watendaji wengine wa chama anashiriki katika kazi za kukiandaa chama kuingia katika uchaguzi mk……” Julius alikatishwa na Mathew.

“Lakini tayari nafahamu kuhusu mpango wa Tanzania mpya na amekiri kuwa ni mshiriki wa mpnago huo.”

“Narudia tena Regina si mshiriki wa Tanzania mpya. *Regina works for Camilla Stewart*” alisema Julius na

kunyamaza baada ya akina Mathew kutazamana.

“Camilla Stewart yupi? Aliuliza Gavana.

“Billionea anayemiliki kampuni kubwa ya Camilla Gold Ltd ambayo inajihusisha na uchimbani na uuzaji wa madini duniani. Ni kampuni ya tatu kwa ukubwa duniani ambayo inajishughulisha na biashara hii ya madini. Kampuni hii imewekeza sehemu mbali mbali duniani na sasa inatafuta nafasi ya

kuingia nchini Tanzania” alijibu Julius.

“Camilla amefariki yapata wiki tatu zilizopita” alisema Gavana.

“Ndiyo. Alifariki kwa ajali ya gari nchini Scotland. *She was killed*.” Julius alinyamaza tena kidogo.

“Tanzania kwa sasa ni kama lulu ya thamani kubwa inayogombaniwa na mabeberu. Mabeberu wanataka kuutumia uchaguzi huu mkuu kupachika watu wao watakaowawezesha

kunufaika na rasilimali zilizopo hapa nchini. Hivi sasa duniani kuna upungufu mkubwa wa madini makubwa kama vile dhahabu, Almasi n.k. Tanzania bado kuna hazina kubwa ya madini hayo ambayo haijaguswa. Hili linawaumiza sana vichwa mabeberu ndiyo maana wanafanya kila wawezalo kuhakikisha wanaweka watu wao madarakani. Camilla alitengeneza mtandao wake ili kumuwezesha kibaraka wake

kushinda uchaguzi. Mmoja wa watu waliokuwa wakifanya kazi katika mtandao huo ni Regina. Alipewa kazi ya kuchunguza kila kinachofanywa na kamati kuu ya Tanzania mpya. Ili kufahamu kile kilichokuwa kinaendelea, ilimlazimu kumchunguza mwenyekiti wake Israel Maungwana kwa kumtumia dereva wake. Dereva huyu alilipwa pesa nyingi sana ili kumfuatilia Israel na kila alichokipata alikuwa anamjulisha Regina.

Hii ni sababu Regina aliweza kufahamu kuhusu mpango wa Tanzania mpya. Israel alipogundua kuwa anafuatiliwa, alitujulisha na kazi ya kumfuatilia Regina tulikabidhiwa SNSA. Tulimfuatilia Regina na kugundua alikuwa anafanya kazi katika mtandao unaofadhiliwa na Camilla Stewart. Ili kuondoa vita na Camilla ambaye mtandao wake ni mkubwa ilitulazimu kutafuta namna ya kumuua

Regina bila kutiliwa shaka kuwa ni sisi ndio tuliofanya mauaji hayo. Camilla ni beberu mwanamke mwenye kuogopwa hadi na mataifa makubwa kutokana na uwezo wake mkubwa na mtandao wake mpana. Kwa kuwa tayari alikuwa na taarifa zetu kutoka kwa Regina, tuliamua kutengeneza mauaji hayo yaonekane yamefanywa na raia kutoka nje ya nchi na yanahusishwa na wivu wa kimapenzi. Hapo ndipo

ulipotengenezwa mpango wa kuwakutanisha Gosu Gosu na Regina” alisema Julius na kunyamaza baada ya Ruby kushituka.

“What?”

“Julius tafadhali…” alisema Mathew na mara Gosu Gosu akasimama.

“It’s true. Anachokisema Julius ni kitu cha kweli kabisa. Niliwahi kuwa na mahusiano na Regina.” alisema Gosu Gosu.

“Jesus !” Ruby alishangaa.

“Nilipewa maelekezo na Joseph Tshibanga ya kuanzisha mahusiano na Regina. Haikuwa rahisi lakini ulitumika ushawishi wa fedha hadi Regina akakubali tukawa na mahusiano ya siri. Mwezi mmoja kabla ya kampeni za uchaguzi mkuu kuanza aliniaga kuwa anakwenda Arusha kwa maandalizi ya uzinduzi wa kampeni za chama chao. Sikujua kama mtu ambaye nilitakiwa kumuua kule Arusha

ni Regina. Nilifichwa siri hiyo hadi pale nilipomshuhudia kupitia lensi ya bunduki. Mwili ulinitetemeka baada ya kugundua mtu ninayetakiwa kumuua ni Regina" alisema Gosu Gosu.

"Gosu Gosu yuko sahihi. Mpango ule ulitengenezwa ili ionekane mauaji ya Regina yanahusishwa na wivu wa kimapenzi. Baada ya mauaji yale Gosu Gosu angetoroshwa nje ya nchi hivyo kuepusha vita kati ya mtandao wa Camilla na

kamati ya Tanzania mpya. Nadhani Mathew umekwisha pata jibu ulilokuwa unalihitaji kwa nini atumike Gosu Gosu kufanya mauji hayo badala ya SNSA. Ni mpango ulioandaliwa kwa umakini mkubwa lakini kwa bahati mbaya haukwenda kama ilivyotakiwa. Baada ya mambo kwenda ndivyo sivyo na Regina kutoweka iligundulika Mathew Mulumbi tayari amekwishalifahamu jambo lile ndipo ukatengenezwa mpango

Regina atafutwe na jeshi la polisi kwa tuhuma za mauaji. Lengo ni ili kumzuia asitoke nchini. Msako mkali ulianza kuwatafuta ninyi pamoja na Regina” alinyamaza Julius.

“Nani waliomuua Camilla? Gavana aliuliza.

“Ilionekana bado Camilla alikuwa hatari kwa mpango wa Tanzania mpya ndiyo maana wakubwa wa mpango huo waliona njia pekea ya kuepusha vita na Camilla ni kumuua. Nchi hizi kubwa

wakikutaka hawakukosi lazima watakumaliza tu na ndivyo ilivyotokea kwa Camilla.” Alijibu Julius.

“Julius pamoja na yote uliyotueleza lakini bado mambo yanakanganya. Israel alileta kwenu suala la Regina na ikaazimia auawe lakini asubuhi ya jana aliwasiliana na Lucy akamtaka amuonye Israel Maungwana asifike msibani kwa kuwa tutakuwepo mahali hapo kumchuguza. Kuna nini

kinachoendelea hapa? Mathew aliuliza.

“Kuna jambo lingine linaloendelea ambalo nitawaeleza pia. Tumalize kwanza suala la mipango ya mabeberu kuhujumu uchaguzi mkuu. Kama nilivyowaeleza kuwa tume ya uchaguzi ni wadau wa Tanzania mpya. Kwa mara ya kwanza mwaka huu watanzania watapiga kura kwa mfumo wa kielektroniki na kuifanya kuwa nchi ya kwanza barani Afrika kutumia mfumo

huo. Mfumo huu ni wa gharama kubwa na fedha zote za kugharamia mfumo wote wa upigaji kura kielektroniki zimetolewa na mabeberu. Hata vifaa vyote vitakavyotumika vimetoka katika kampuni ya moja ya nchi wanaofahili mpango wa Tanzania mpya. Hii ni katika kuhakikisha mpango wao unafanikiwa. Baada ya watanzania kupiga kura mchezo wote wa kukiondoa madarakani chama kinachotawala na kukiweka

chama cha ukombozi wa Afika utachezwa hapa katika mfumo huo. Usiku wa kuamkia jana wameingia nchini watu watatu ambao wanatoka katika kampuni iliyotengeneza vifaa na mfumo mzima utakaotumika katika upigaji kura kielektroniki. Wanakuja kucheza na mfumo huo ili kumuwezesha mgombea wa chama cha ukombozi wa Afrika kuibuka mshindi kwa kupata kura nyingi katika uchaguzi mkuu. Hivi tuzungumzavyo

watu hao tayari wako sehemu wanakutana na mwenyekiti wa tume ya uchaguzi kwa siri ili kujadili namna watakavyoweza kucheza na mfumo huo. Jamani mambo yameiva. Hawa watu hawataki utani kabisa katika mambo yao. Wamejiandaa na wanachokizungumza wao ni mafanikio tu hawana msamiati wa kushindwa. Muamini msiamini lakini huo ndio ukweli. It's happening" alisema Julius na kuwatazama akina

Mathew. Joto lilionekana kupanda ndani ya kile chumba. Julius baada ya kupumzisha koo kwa sekunde chache akaendelea kumwaga mambo.

“Kwa kuwa mwenyekiti wa tume ya uchaguzi ni mmoja wa wadau wa Tanzania mpya, hakutakuwa na uchelewesha ji wa kutangazwa matokeo. Mshindi atatangazwa haraka na kwa mujibu wa katiba yetu ushindi wa Rais haupingwi mahakamani basi atakapotangaza kila kitu

kitaishia hapo. Nchi itaingia katika mikono ya mabeberu” alisema Julius.

“Mathew I need a drink.” alisema Gosu Gosu huku akiinuka

“No!. Hatuna muda wa kukusubiri. Endelea Julius” alisema Mathew na Gosu Gosu akaketi.

“Mh ! Sikutegemea kama jambo hili ni kubwa kiasi hiki” alisema Gavana.

“Mzee, laiti ungejua namna mabeberu wanavyoiwaza nchi hii ungelia machozi. Ipo mikakati mingi ya kuingia Tanzania kuchuma rasilimali na kama zisipofanyika juhudi za makusudi basi watafanikiwa mipango yao.”

“As long as I still breathing hakuna mpango wowote wa mabeberu na vibaraka wao utakaofanikiwa. Endelea Julius. Muda unakwenda mbio” Alisema Mathew.

“Usiku wa leo ameuawa jaji mstaafu Perfect Lyimo. *SNSA killed him”* alisema Julius na kunyamaza akawatazama akina Mathew.

“Why you killed him? Aliuliza Ruby .

“Tuligundua tayari mnafuatilia mawasiliano yake, vile vile alikuwa na mahusiano na Ambola ambaye tayari ilikwisha gundulika alikuwa upande wenu. Hakukuwa na namna nyingine ya kufanya zaidi ya kumuua. Lengo

lilikuwa kuwadhibiti msiweze kupata chochote kutoka kwake. Mpango ulikuwa kumuondoa Ambola pia lakini kuna makosa yalifanyika na kuharibu mpango mzima.” Julius aliwaeleza kile kilichotokea hadi alipopigiwa simu na Charles Ombe akajulishwa kuhusu mpango wa kumuua.

“Charles Ombe naye ni mshirika wa Tanzania mpya? Mathew aliuliza.

“Ndiye mwenyekiti wa kamati hiyo ya Tanzania mpya”

“Ninafahamiana naye sana.” Alisema Mathew.

“Ninamshukuru Charles kwani dakika chache baada ya mimi kuondoka eneo la tukio walifika watu ambao walitumwa kuniua wakanikosa. Charles alinishauri baada ya kunusurika katika mtego huo wa kuuawa nikimbie nchi. Baada ya kutafakari kwa kina sijaona sababu ya kukimbia nchi. Nimeamua kubaki hapa nchini nipambane na hawa watu wanaotaka kuniua.

Nimekuja kwenu na kuwaelexza kila kitu kinachoendelea ili tuunganishe nguvu na kuhakikisha mipango yote miovu ya hawa jamaa haifanikiwi.” Alisema Julius. Ulipita ukimya wa sekunde kadhaa halafu Gosu Gosu akasimama na kusema.

“Umetueleza haya yote baada ya maisha yako kuwa hatarini. Kama si kutakiwa kuuawa ungeendelea kuwa sehemu ya mashetani wanaopanga njama ovu dhidi

ya taifa hili. Kama umewasaliti wenzako unategemea nasi tutakuamini? Aliuliza Gosu Gosu. Sura yake ilijaa hasira. Alionekana kuna kitu kinamsumbua kichwani.

“Watu hubadilika na hata mimi mwenyewe sikujua kama ningeweza kubadilika na kuwa namna hii. Sikutegemea kama siku moja ningekaa nanyi chumba kimoja tukizungumza. Ninyi mlikuwa maadui zangu na kazi yangu ilikuwa ni kuwasaka na kuwaua lakini

maajabu ya Mungu muda huu niko na adui zangu tunazungumza masuala ya kitaifa. Naomba mniamini ndugu zangu haya ninayowaambia ni ukweli mtupu.”alisema Julius.

“Unaniudhi unapotuita sisi ndugu zako….” Alisema Gosu Gosu ikamlazimu Mathew kuingilia kati.

“Gosu Gosu pamoja na yote yaliyotokea lakini Julius ametufumbua macho. Kama anavyosema watu hubadilika.

Kwa sasa bado kuna mengi ambayo tunahitaji kuyasikia kutoka kwake hivyo tumpe nafasi. Julius ahsante sana kwa haya uliyotueleza lakini bado tunaendelea kukusikiliza. Tueleze kila kitu na baada ya hapo tutapata wasaa wa kujadili kwa pamoja hatua za kuchukua."

"Ahsante Mathew. Bado kuna mengi ya kuwaeleza lakini kabla sijaendelea ninataka kufahamu kile walichoeleza Lucy na Regina

baada ya kuwahoji. Naamini kuna mambo wamewaambia.” alisema Julius. Mathew alimweleza kile walichokisema Regina na Lucy walipohojiwa.

“Alichokisema Regina ni kweli. Anafanya kazi katika kampuni ya utafiti madini ya Termo. Kampuni hii mmiliki wake ni Sophia Mnambara mke wa Rais mstaafu Malaki Mnambara. Kampuni hii ilianzishwa baada ya vifo tata vya bilionea Albert na mwanae Sixmund ambao ni baba na

kaka wa Sofia. Haya yote tayari mmeelezwa na Lucy lakini naomba niongezee kidogo. Kuna mambo ambayo hawajayasema aidha kwa kuficha au kutofahamu.” Alisema Julius.

“Endelea” Mathew alitoa ruhusa.

“Lucy amewaeleza kuhusu vifo tata vya bilionea Albert Wengela na mwanaye Sixmund Wengela ambaye alikuwa waziri wa fedha katika serikali hiyo. Ilimlazimu Sophia

mnambara kutafuta wapelelezi wa kujitegemea kutoka nje ya nchi ili kuchunguza kuhusiana na vifo hivyo. Taarifa aliyopewa Sophia ilionesha SNSA wanahusika na mauaji hayo. Sophia aliamua kuunda kampuni hiyo ya madini ya Tarmo ili kulipiza kisasi kwa wale wote waliohusika katika mauaji ya baba na kaka yake. Taarifa mpya ya uchunguzi baada ya Tarmo kuanzishwa ilionesha SNSA hawakuhusika katika mauaji hayo ya bilionea

Albert na mwanaye Six. Iligundulika mauaji hayo yalifanywa na kundi linajulikana kama *Kumi 255*." Alinyamaza kidogo kisha akaendelea.

"*Kumi 255* ni kundi hatari sana ambalo asili yake ni kundi la *Kumi 415* lililoanzia katika gereza la Folsam nchini Marekani. Mmoja wa watu waliowahi kufungwa katika gereza hilo na akawa mshiriki wa genge hilo la *Kumi 415* ndiye aliyeanzisha kundi la

Kumi 255. Kundi hili lina idara kumi ndani yake na Kila idara ndani ya kundi hili ina watu kumi pekee. Hii ni sababu likaitwa *Kumi 255*. Ni kundi hatari sana hili na ambalo lilitumiwa kufanya mauaji ya Bilionea Albert na mwanaye Sixmund."

"Ni mara ya kwanza ninasikia kuhusu uwepo wa kundi hilo" alisema Gosu Gosu.

"Huwezi ukalifahamu kwani ni kundi la siri sana." alisema Julius, akanyamaza

kwa muda kidogo halafu akauliza.

“Kwa nini Bilionea Albert na mwanaye Sixmund waliuawa?

Hakuna aliyekuwa na jibu la swali lile.

“Bilionea Albert Wengela aliwahi kutajwa miongoni mwa matajiri watano wakubwa ndani ya bara la Afrika. Nguvu yake ya pesa na ushawishi ilimsaidia Malaki kuingia ikulu. Inasemwa utajiri wa Albert uliongezeka mara dufu

baada ya Malaki kuingia ikulu. Mgogoro ulianza baada ya Albert kumjulisha Rais Mnambara kuwa alipata taarifa za uwepo wa ramani muhimu sana ya Tanzania ambayo inaonesha aina zote za madini yaliyopo Tanzania, mahali yalipo na kiasi kilichopo. Ramani hiyo ilitengenezwa kwa siri kubwa na nchi moja kubwa yenye uwezo mkubwa kiteknolojia. Ramani hiyo inaonesha Tanzania kuwa na hazina kubwa sana ya madini

ambayo mengine bado hayajafahamika na serikali kama yapo nchini. Ramani hiyo ndiyo iliyowapa wazimu mabeberu hao kufanya kila namna ili waweze kuingia nchini na kufaidika na rasilimali hizo. Baada ya kushauriana walikubaliana kufanya mpango ili waweze kuipata ramani hiyo ambayo ingewawezesha kupata utajiri mkubwa. Hapo ndipo lilipotokea kundi la *Kumi255*. Kundi hili ambalo asilimia

themanini ya watu wake wana mafunzo ya ujasusi waliingia katika nchi hiyo hadi mahali ilikofichwa ramani wakaichukua na kuja nayo Tanzania. Haikuwa ramani moja bali ramani tatu. Ramani ya Tanzania, ya Afrika na ramani ya dunia. Ramani zote tatu zikionesha uwepo wa madini mbali mbali katika kila nchi.” Julius alinyamaza kidogo 6kwa sekunde chahe halafu akaendelea.

“Mikakati mizito ilipangwa kati ya Rais Mnambara na Albert namna ya kufaidika na ramani ile kwa kujimilikisha kwa siri maeneo yote yenye madini na kuanza uchimbaji kwa siri. Kabla mikakati hiyo haijakamilika ramani hizo ziliibwa kutoka mahali zilikohifadhiwa. Uchunguzi mkali ulifanywa akafahamika aliyechukua ramani hizo ambaye alikuwa mmoja wa walinzi ambao Rais alimpa bilionea Albert. Mtu huyo

alikamatwa akateswa na kuuawa lakini hakuonesha mahali zilipo ramani hizo.” alisema Julius na Mathew akasimama.

“Naomba mnisbiri kwa dakika mbili” alisema Mathew akainuka na kutoka mle ndani akaenda katika chumba alimo Ambola. Alifungua mlango na kumkuta Ambola amejilaza katika sofa.

“Mathew” alisema Ambola.

“Ambola unaendeleaje? Aliuliza Mathew.

“Ninaendelea vyema kwa sasa. Tayari nimepumzika vya kutosha.”

“Good. Endelea kupumzika.”

“Ahsante sana Mathew. Nini kinaendelea huko?

“Ambola nitazungumza nawe baadaye kidogo lakini kwa sasa kuna kitu nahitaji kufahamu kutoka kwako. Baba yako aliitwa nani?

“Aliitwa Julius Kabembo”

“Ahsante” alisema Mathew na kutoka mle ndani akarejea katika chumba walimo wenzake.

“Julius huyo mtu ambaye aliiba ramani hizo mahali zilikohifadhiwa jina lake ni Julius Kabembo? Aliuliza Mathew na kumshangaza Julius.

“Ndiyo. Kumbe unamfahamu”

“Endelea” alisema Mathew.

“Mathew yuko sahihi. Mtu aliyeiba ramani hizo ni Julius Kabembo. Mgogoro kati ya Rais na Albert ulianzia hapo. Rais Mnambara aliamini amezungukwa na Albert na mwanaye Sixmund ambaye walimshirikisha katika mpango ule. Baada ya kuzitafuta ramani zile bila mafanikio ndipo Rais Mnambara alipoamua kuwamaliza Albert na mwanaye Sixmund akilitumia kundi hatari la mauaji la *Kumi255*. Mauaji

hayo ndiyo yaliyopelekea Sophia kuanzisha kampuni ile ya madini ya Tarmo. Kampuni ile hakuisajili kwa jina lake bali ilisajiliwa kwa jila la rafiki yake wa karibu ambaye ni Lucy mke wa Gavana.”

“Siamini kama mwanamke huyu anaweza kufanya mambo kama haya bila mimi kujua. Ama kweli jambo hili limenifumbua macho. Sikujua kama ninalala kitanda kimoja na kiumbe hatari mno. Dah !” alisikitika Gavana.

“Si hilo tu kuna mengi amekuficha. Baada ya kugundulika kuwa ni *Kumi 255* waliofanya mauaji yale, Sophia aliuona mlima mrefu wa kupanda. Asingeweza kupambana na kundi lile hatari ambalo lilikuwa linatumiwa na mumewe Malaki. Aliamua kubadili mawazo. Aliamua kutafuta kwanza nguvu ya kutosha ili kupambana na watu waliomuua baba yake. Alianza kutengeneza mtandao ili mmoja wa ndugu zake apate

nafasi ya kugombea urais kupitia chama kinachotawala. Mipango yake ilifanikiwa na binamu yake akafanikiwa kupitishwa na chama tawala ili awanie urais. Huyo ndiye anayeshindana na mgombea wa chama cha ukombozi wa Afrika. Kuna jambo ambalo yawezekana hamlifahamu bado.” Alinyamaza kwa sekunde chache.

“Nina undugu na Sophia Mnambara. Alihitaji kuwa na mtu ndani ya idara ya SNSA

hivyo nilifanikiwa kupata nafasi hiyo nikaingia SNSA. Baada ya Faraji Mnambara kutolewa, nilipewa mimi nafasi yake nikawa mkurugenzi wa SNSA moja kwa moja nikajumuishwa katika mpango wa Tanzania mpya na mambo yote yaliyotokea nimewaeleza hadi walivyonigeuka na kutaka kuniua. Ndugu zangu nchi hii inagombaniwa kama mpira wa kona. Hata Sophia Mnambara naye kuna watu kutoka nje ya nchi wako nyuma yake

kuhakikisha mtu wao anashinda uchaguzi ndiyo maana aliweka mtu ndani ya SNSA kufuatilia kile kinachofanywa na idara hiyo kukisaidia chama cha Ukombozi wa Afrika kushinda uchaguzi. Mtu huyo ni mimi hapa. Ninafanya kazi SNSA lakini hapo hapo niko katika kampuni ya Tarmo. Tumetengeneza utatu yaani Regina, Lucy na mimi. Regina anachunguza kila kinachoendelea ndani ya

chama chake. Atakachokipata anakiwasilisha kwa Lucy ambaye naye hukiwasilisha kwangu. Hatuna mawasiliano ya moja kwa moja kuogopa kugunduliwa.”

“Unatuchanganya we jamaa. Umesema Regina na Lucy uko nao pia katika kampuni ya Tarmo inayomilikiwa na Sophia. Ulifahamu mpango wa kumuua Regina kwa nini hukumsaidia? Kwa nini hukumjulisha kama atauawa?

Ulikuwa tayari mwenzako auawe? Aliuliza Gosu Gosu.

“Sikufanya hivyo kwasababu kama Regina angejua kuna mpango huo wa kumuua angekimbia na kuwashitua wale jamaa ambao wangejua lazima kuna mtu kavujisha siri. Sikutaka washituke ndiyo maana sikumjulisha Regina chochote.”

“Mtandao wa Tanzania mpya wanafahamu uwepo wa timu ya siri inayomsaidia

mgombea wa chama tawala na inayofahamu mambo yao?” Mathew aliuliza.

“Hapana hawafahamu chochote. Wanachoamini wanapambana na chama tawala hawajui kama kuna timu ya siri ambayo mimi ni mshiriki wake.”

“Mtandao wa Sophia Mnambara nao wamefikia wapi katika mipango yao kuhakikisha mgombea wao anashinda uchaguzi? Mathew aliuliza.

“Hofu yao kubwa ni hawa Tanzania mpya. Kwa sasa wanaendelea kufuatilia kwa karibu sana kila kinachofanywa na mtandao wa Tanzania mpya. Mimi ni jicho lao ndani ya Tanzania mpya hivyo ninawajulisha kila kinachoendelea. Kitu pekee ambacho hawakifahamu bado ni ujio wa wale wataalamu watatu ambao wamekuja kucheza na mfumo wa upigaji kura wa tume ya uchaguzi. Hata mimi jambo hilo

nimelifahamu usiku huu tukiwa katika kikao. Mpango huo ulifanywa siri na hata m wenyekiti mwenyewe amejulishwa usiku huu pia na Israel Maungwana kuhusu ujio wa hao watu kwani yeye ndiye aliyewaleta watu hao."

"Israel ndiye aliyewaleta watu hao? Mathew aliuliza.

"Ndiyo. Kuna jambo ambalo sikuwaeleza hapo kabla. Israel Maungwana ndiye kiongozi wa kundi hatari la

Kumi255.” Alisema Julius na ukimya ukatanda.

“Julius nataka kufahamu nini mipango ya kampuni yenu katika kuvuruga mpango wa Tanzania mpya? Gavana aliuliza.

“Bado haijaamriwa nini kifanyike. Bado tunaendelea kufuatilia mipango yao ili tujue nini kifanyike” alijibu Julius.

“Bado hujajibu swali nililokuuliza kwa nini Regina alimtaka Lucy akupe taarifa umuonye Israel asifike msibani

nyumbani kwa Bernadetha? Kwa nini hakutaka tufahamu kama Israel na Bernadetha wana mashirikiano? Mathew aliuliza.

“Kwa sababu ndani ya Tarmo bado tuna misheni maalum ya kumchunguza Israel na kundi lake la *Kumi255*. Bado Sophia anataka kulipiza kisasi kwa Israel na kundi hilo. Tulihofu kama mngefahamu Israel ana mahusiano na Bernadetha mngeanza kumchunguza na

kuharibu kile tunachokitafuta kwake”

“Tayari mmefahamu anaongoza kundi la *Kumi 255*, anashiriki katika mpango wa Tanzania mpya. nini kingine mnakichunguza kwake? Mathew aliuliza.

“Kuna mpango wa kuleta machafuko makubwa endapo itatokea kwa namna yoyote ile chama cha ukombozi wa Afrika kikashindwa katika uchaguzi. Huo ni mpango wa siri kubwa

ndiyo maana tunamuhitaji sana Israel.”

“Ulimjulisha Israel kuwa nitakuwepo msibani? Mathew aliuliza.

“Sina mawasiliano ya moja kwa moja na Israel. Yule ni mtu ambaye hapendi kufanya urafiki na watu asiowafahamu. Nilimtumia mwenyekiti Charles ili amtake Israel asifike msibani kwa sababu za kiusalama. Sikumwambia kama Mathew atakuwepo msibani.”

“Mnamtafuta Regina na ulifahamu yuko nasi na ungeweza kuwajulisha wenzako kwa nini hukufanya hivyo? Aliuliza Gosu Gosu.

“Sikufanya hivyo kwa sababu Regina ni mwenzangu na sikutaka ajulikane mahali alipo”

“Alfajiri ya leo, kwa kusaidiwa na Lucy mlimteka Gavana mkampeleka kusikojulikana mkataka awaeleze mahali mimi na wenzangu tulikojifi…….”

Alisema Mathew na kabla hajamaliza Julius akasema.

“Kile kilikuwa kiini macho. Nilitaka kuwaonesha wenzangu kuwa tunapiga hatua katika kumsaka Mathew Mulumbi ndiyo maana tulimteka Gavana. Hata kama Gavana angeonesha mahali mlipo nisingethubutu kufikisha taarifa hiyo kwa kamati kwa kuwa Regina alikuwepo mahali hapo.”

“Bastard !” alifoka Gavana akasimama na kumnyooshea Julius kidole.

“Nimeteswa sana na watu wako. Nimedhalilishwa na vijana wadogo halafu unadiriki kutamka eti ilikuwa ni kiini macho. Bazazi mkubwa we !” alifoka Gavana aliyepandwa na hasira za ghafla.

“Nisamehe mzee wangu lakini ilikuwa lazima upitie mteso yale ili wenzangu wajue kuna kazi inafanyika.” Alijitetea Julius.

“Tubaki hapo hapo kwa Gavana. Mwanae Kelvin tumepata taarifa alikuwa ni mpelelezi wa siri wa SNSA. Gavana anaamini Regina kuna kitu anafahamu kuhusu kutoweka kwa Kelvin. Mpaka sasa Gavana ameweka wapelelezi watatu ili kumchunguza Regina na kutafuta majibu kuhusu kutoweka kwa Kelvin lakini wapelelezi hao wote watatu wamekuwa wakiuawa. Mara ya mwisho alikuwa ni mpelelezi

kutoka Zambia ambaye alitumwa kumchunguza Regina lakini mligundua mkamuua. Nataka kujua ni namna gani mnagundua kuhusu wapelelezi hao na kwa nini mnawaua?

"Kila Gavana anapoweka mpelelezi kumchunguza Regina tunajulishwa na Lucy na tunamuua. Kuna sababu mbili. Moja ni kuepusha Regina kugundulika kama ni mpelelezi. Pili ni kuficha ukweli kuhusu kutoweka kwa

Kelvin kwani ni kweli Regina anafahamu kila kitu kuhusu Kelvin”

“Umefika mwenyewe ninapopataka. Kwa muda mrefu sasa nimekuwa nikitafuta mtu anayefahamu ukweli kuhusu kutoweka kwa mwanangu na hatimaye leo umepatikana. Nataka kufahamu kila kitu kuhusu mwanangu tafadhali.” alisema Gavana.

“Gavana nilikuahidi kukueleza kila kitu kuhusu

Kelvin na huu ndio ukweli” Julius alinyamaza kidogo akamtazama Gavana ambaye mapigo ya moyo wake yalikuwa yanakwenda kwa kasi kubwa.

“Kelvin is alive” alisema na kunyamaza tena. Midomo ya Gavana ilitetemeka.

“Wh…where is he?” aliuliza huku sauti yake ikiwa na kitetemeshi.

“Nimewaeleza kuhusu kampuni ya Tarmo. Kelvin alikuwa mmoja wa watu wa

mwanzo kufanya kazi katika hii kampuni. *He was double agent*. Alifanya kazi SNSA na wakati huo huo alikuwa katika kampuni ya Tarmo. Baadaye alipewa kazi ya kuchunguza kuhusu minong'ono iliyoanza kuvuma kuhusu kifo chenye utata cha Rais mstaafu Malaki Mnambara. Alifanya uchunguzi huo kwa siri akishirikiana na Faraji Dilele aliyekuwa mkurugenzi wa SNSA wakati huo. Kelvin alifanya uchunguzi huo kimya

kimya na aliupata ukweli kuhusu Malaki Mnambara lakini kabla hajauwasilisha kwa mkuu wake, alitoweka kwa namna ya ajabu sana na hadi sasa watu hawajui mahali aliko. Wengi wanaamini alikufa maji japo mwili wake haujawahi kupatikana. Ukweli ni kwamba Kelvin alifanikiwa kuupata ukweli kuhusu Rais mstaafu Malaki Mnambara kuwa hai lakini kitendo hicho kiliyaweka maisha yake hatarini hivyo kumlazimu

kutengeneza tukio lile la kutoweka ili kunusuru maisha yake kwani alitakiwa kuuawa.”

“Nani waliotaka kumuua?

“Israel Maungwana ni mshirika mkubwa wa Malaki. Pamoja na jukumu lake la mwenyekiti wa chama lakini ana jukumu lingine la kuhakikisha anailinda kwa nguvu zote siri ya Malaki Mnambara kuwa hai. Kelvin akiwa katika harakati za kusaka ukweli kuhusu Malaki Mnambara, ilimlazimu

kuanzisha mahusiano na Rosana Mnambara mtoto wa Malaki. Kupitia kwake ndipo aliufahamu ukweli kwamba Rais Mnambara yuko hai. Israel na kundi lake la Kumi 255 ndio wanaomlinda Malaki kuhakikisha anakuwa salama hivyo waligundua kile alichokuwa anakifanya Kelvin na kupanga kumuua. Ni Rosana aliyemshitua Kelvin kuhusu mpango wa kumuua. Kelvin alitoweka ili kulinda uhai wake.”

“Where is he now?
Unafahamu mahali aliko?” aliuliza Gavana.

“Kelvin yuko hapa Dar es salaam lakini kuna mtu mmoja tu nayefahamu mahali aliko naye ni mke wako Lucy”

Gavana macho yalimtoka.

“Rucy anafahamu jambo hili? Gavana aliuliza sura yake ikiwa imetawaliwa na mshangao mkubwa.

“Ndiyo mzee. Mkeo Lucy ndiye anayefahamu mahali aliko Kelvin”

“Ee Mungu kwa nini ukakubali niishi na kiumbe hatari kama huyu? Kwa muda mrefu nilijua niko na mwenzangu kumbe ninaishi na kiumbe hatari.” Gavana alisikitika. Aliinuka na kwenda kujiegemeza ukutani. Kichwa chake kilijaa mawazo.

“Kuna jambo lingine la muhimu ambalo mnapaswa kulifahamu.” Alisema Julius.

Gavana aligeuka aliposikia kuna jambo lingine.

“Ni jambo gani hilo Julius? Mathew aliuliza.

“Mimi, Lucy, Regina na Kelvin tuna operesheni ya pamoja.” Alisema Julius na kila mmoja mle ndani alionesha sura ya mshangao.

“Julius unatuchanganya na taarifa zako. Umesema hujui mahali aliko Kelvin halafu unadai mna operesheni ya pamoja. Lipi tuliamini? Mathew aliuliza.

“Ni kweli sifahamu mahali aliko Kelvin lakini tunashirikiana naye katika operesheni ya siri.”

“Inahusiana na nini hiyo operesheni? Mnaiendesha vipi? Mathew aliuliza.

“Ni mpango wa kuzuia hiki kinachoendelea hivi sasa yaani mipango ya mabeberu kuvuruga uchaguzi wetu mkuu” alisema Julius na kumtazama Mathew.

“Najua nimewachanganya kwa haya mambo

niliyowaeleza. Naomba nifafanue. Mimi kama mkurugenzi wa SNSA niko oh sorry nilikuwa katika kamati ya Tanzania mpya. Niko pia katika kampuni ya Tarmo ambao wao mipango yao ni kuhakikisha mpango wa Tanzania mpya haufanikiwi lakini mtu wao ambaye ni mgombea urais wa chama kilichopo madarakani anashinda uchaguzi. Mimi ni jicho lao ndani ya SNSA na katika kamati ile ya Tanania

mpya. Wakati haya yakiendelea Kelvin kupitia kwa mama yake Lucy, alikuja na mpango maalum wa kuhakikisha mipango yote ya makundi haya mawili na mengine ya mabeberu haifanikiwi.”

Mathew alivuta pumzi ndefu na kuuliza.

“Namna gani mnaitekeleza operesheni hiyo?

“Kelvin ndiye mwenye kutoa maelekezo yote lakini kwa sasa tunaendelea na zoezi

la kukusanya taarifa mbali mbali za mipango yote ya makundi haya mawili, baada ya hapo tutaona nini cha kufanya kuzuia mipango hio isifanikiwe”

“Mathew mtaendelea kumuhoji huyu mtu mambo yenu, mimi kwa sasa nataka yule mwanamke anioneshe alipo mwanangu. Ni hicho tu ninachokihitaji” alisema Gavana.

“Mzee tayari umefahamu kuwa mwanao yuko hai na

yuko hapa Dar es salaam. Usihofu utaonana naye lakini kwa sasa tunaendelea na masuala muhimu ya kitaifa. Tukimaliza hapa tutahamia katika suala hilo.”

“Oh my God! Alisema Gavana na kukaa chini. Alichanganyikiwa.

“Julius nataka kufahamu kuhusu uhusika wa Lucy katika mpango wa Tanzania mpya kwani ulimtumia ujumbe kumjulisha kuhusu kifo cha Bernadetha.”

“Katika mpango wa Tanzania mpya, Lucy ni mmoja wa wale watu wa mwisho kabisa ambao wanajulikana kama watoa taarifa. Ni mimi niliyelipeleka jina lake mbele ya kamati na kumtambulisha kama mmoja wa watoa taarifa.”

“Taarifa gani ambazo unazihitaji kutoka kwake hadi ukaamua kumshirikisha katika mpango huo? Aliuliza Mathew.

“Taarifa kubwa ambayo niliihitaji kutoka kwa Lucy ni

kuhusiana na wapelelezi ambao Gavana amekuwa akiwaweka ili kumchunguza Regina.” Alijibu Julius na Gavana akainua uso wake akamtazama kwa hasira.

“Unafahamu ni gharama kiasi gani niliitumia kuwakodisha wapelelezi wale ambao mliwaua? Alifoka Gavana.

“Mzee, utanisamehe kwa kuwaua wapelelezi hao lakini ilitulazimu kufanya hivyo kwani bila kufanya hivyo

ingehatarisha usalama wa operesheni zetu na ingehatarisha pia usalama wa Kelvin.”

“Mabazazi wakubwa nyie! Alisema Gavana kwa hasira.

“Mzee kuna jambo ambalo unapaswa kulifahamu kuhusu mkeo Lucy. Huyu aliwahi kufanya kazi katika shirika la ujasusi Tanzania. Amefanya kazi katika nchi za Afrika kusini, Somalia, DR Congo, na Msumbiji.”

“Nilikutana naye katika ndege nikitokea nchini Afrika kusini. Mahusiano yetu yalianzia hapo.” Alisema Gavana.

“Wakati huo tayari alikuwa anafanya kazi katika shirika la ujasusi Tanzania” alisema Julius.

“Mimi nilifahamu kazi aliyokuwa anaifanya ni afisa katika kampuni moja inayojishughulisha na uagizaji wa mafuta hapa nchini. Ni kutokana na kazi hiyo

amekuwa akisafiri mara kwa mara kumbe safari hizo zote amekuwa akienda katika kazi zake. Julius kama kuna mengine kuhusu Lucy tafadhali naomba usiniambie nitakufa. Haya uliyonieleza yananitosha kwa sasa.” Alisema Gavana.

“Mzee huu ni muda wa kuufahamu ukweli wote. Kama kuna jambo lingine linalohusiana na mkeo Lucy lazima uwe tayari kulipokea.” Alisema Mathew.

“Mathew sihitaji zaidi ya hapa. Sitaki kufa kabla ya wakati wangu. Kwa haya aliyonifanyia sina mpango wa kuendelea naye tena.”

“Mzee nakusihi usimlaumu sana mkeo kwa kile alichokifanya kukuficha ukweli kuhusu yeye. Amefanya hivi si kwa ridhaa yake bali ni misingi ya hizi kazi. Hutakiwi kumweleza mume, mke au mpenzi wako kuhusiana na kazi yako. Hii ni kwa ajili ya usalama wako mwenyewe.”

Alisema Mathew na kumgeukia Julius.

“Julius nataka kufahamu kuhusu Regina. Alikuwa na mpango wa kukimbilia katika kisiwa cha Zales kwenda kujificha. Huu ulikuwa mpango wenu?

“Regina ana fedha nyingi zimefichwa katika kisiwa cha Zales ambazo alilipwa na mtandao wa Camilla kama nilivyowaambia alikuwa anawafanyia kazi. Fedha hizo zimewekwa katika akaunti

maalum kisiwani Zales. Baada ya haya mambo kutokea tulitaka kumuondoa hapa kwenda kisiwani huko hadi hapo mambo yatakapotulia” alijibu Julius. Kilipita kimya cha sekunde chache Mathew akauliza.

“Julius kuna lingine ambalo bado tunahitaji kulifahamu? Aliuliza.

“Mathew nimewaeleza kila kitu. Nilimweleza Gavana kuwa jambo hili ni kubwa na akina Mathew wanatakiwa

walifahamu kwa undani. Ninachokihitaji kwa sasa ni kushirikiana nanyi kuhakikisha mipango ya hawa jamaa haifanikiwi.” alisema Julius.

“Julius nina swali kwako” alisema Gosu Gosu.

“Haya uliyotuleza ni mambo mazito ya siri na mengi hatukuwa tukiyafahamu. Nataka kujua kwa nini umechukua maamuzi ya kutueleza sasa mambo haya?”

“Ni kwa sababu mimi si sehemu yao tena. Nimekuwa

adui yao hivyo namna pekee ya kupambana nao ni kuungana nanyi ndiyo maana nimewaeleza kila kitu bila kuwaficha”

“You want us to fight your war. Kama kusingekuwa na mpango wa kukuua basi ungendelea na jitihada zako ukishirikiana na vibaraka wa mabeberu kutusaka na kuzuia mipango yetu mizuri. Kama kusingekuwa na mpango wa kukuua huyu mzee ambaye mmemtesa kuanzia asubuhi

asingekuwa hai hivi sasa pengine mngekwisha muua. Unataka kuungana nasi tutakuaminije? Kama umeweza kuwasaliti wenzako utashidwaje kutusaliti na sisi pia? Aliuliza Gosu Gosu.

“Ndugu zangu hakuna sababu ya….”

“Usituite ndugu zako !alifoka Gosu Gosu.

“Gosu Gosu mpe nafasi ya kujieleza.”alisema Mathew.

“Japo Gosu Gosu hataki niwaite ndugu lakini ninyi ni ndugu zangu kwa sababu sote tunajenga nyumba moja. Sote nia yetu ni moja kuinusuru nchi yetu kuingia katika mikono ya mabeberu. Kama ningekuwa na malengo mabaya kwenu ningekwisha wafanyia jambo baya wakati nikiwa SNSA kutokana na uwezo mkubwa wa idara ile. Nasema hii yote ni mipango ya Mungu kutukutanisha ili tuungane na

kuwa kitu kimoja.” Alisema Julius.

“Julius kuna chochote kingine bado unacho cha kutueleza? Mathew aliuliza.

“Nimewaeleza mambo yote muhimu ambayo nilidhani ni muhimu mkayafahamu. Kama kuna mengine nitaendelea kuwaeleza”

Kilipita kimya cha sekunde ishirini. Kila mtu alikuwa anatafakari baada ya maelezo marefu na mazito kutoka kwa Julius.

“Julius” alisema Mathew na kuwaondoa watu wote mle ndani katika mawazo waliyokuwa nayo.

“Nakubaliana nawe kuwa kukutana nawe ni maongozi ya Mungu. Kupitia kwako tumefahamu mambo mazito ambayo pengine ingetuchukua muda kuyajua japo tulikuwa katika mwelekeo mzuri wa kuyafahamu haya yote uliyotueleza. Uliyotueleza ni mengi tunahitaji kupata wasaa wa kuyachambua na kuona ni

namna gani tunaweza kuyafanyia kazi. Ndugu zangu maelezo haya ya Julius yametupa picha kuwa nchi yetu ni kama Swala mnono aliye katikati ya kundi la Mbwa mwitu wenye njaa kali. Nchi yetu imebarikiwa utajiri mkubwa sana na hivyo kumezewa mate na mabeberu wenye uchu na rasilimali zetu. Yamekuwa ni mashindano kati ya mabeberu nani ataibuka mshindi na kumuweka kibaraka wake madarakani.

Inaumiza sana kwa washenzi hawa kushindwa hata kuheshimu uhuru wetu. Binafsi ninasema tutailinda nchi yetu. Huu ni wakati wetu wa kusimama imara na kuipigania nchi yetu kuhakikisha haitumbukii katika mikono ya mabeberu. Tumemsikia Julius alivyotuambia kuwa kumeandaliwa hadi machafuko pale ambapo kundi Fulani litakaposhindwa uchaguzi. Yote hii ni katik akufanikisha

mipango ya mabeberu. Hawa watu ni wanyama sana” alinyamaza Mathew na kumtazama Gavana aliyekuwa anafuta machozi. Baada ya sekunde chache akaendelea.

“Kitu kikubwa ambacho tunahitaji kukifanya kwanza ni kuunganisha nguvu. Tunapambana na watu hatari sana ambao wengine tayari wamekita mizizi yao hadi ndani kabisa ya serikali. Naweza kusema serikali yetu imegawanya vipande vipande

na mabeberu wenye uchu wa kumuweka kibaraka wao madarakani kupitia uchaguzi mkuu unaokuja. Hatupambani na kundi moja. Julius ametueleza kuna makundi matatu anayoyafahamu. Kundi la Tanzania mpya ambao ndani yake kuna kundi la *Kumi255*. Kundi la pili ni la Sophia Mnambara ambaye naye anamuunga mkono mgombea mwingine. Kundi lingine la tatu ni kundi la blionea Camilla ambao nao wana chama

wanachokiunga mkono. Hayo ni makundi matatu ambayo Julius anayafahamu lakini naamini yapo makundi mengine zaidi kwani kama nilivyowaeleza nchi yetu ni kama Swala aliyenona mbele ya kundi la Mbwa mwitu. Nchi yetu inataka kurararuriwa vipande vipande. Wa kuikoa nchi yetu katika hatari hiyo ni sisi hapa.”

“Inasikitisha sana Mathew kwa haya tunayofanyiwa na hizi nchi kubwa. Kwa nini

wanashindwa kuheshimu uhuru wetu hadi wanatufanyia mambo haya machafu?” Aliuliza Gavana.

“Kikubwa kinachosababisha haya yote kutokea ni uwingi wa rasilimali tulizonazo. Mabeberu hawapotezi muda wao katika nchi ambayo hawatafaidika na chochote. Mabilioni ya fedha yamemwagwa hapa nchini katika uchaguzi huu mkuu kwa sababu wana uhakika watafaidika na utajiri mkubwa

tulio nao. Akitokea mtu au kundi la watu kutaka kuharibu mipango yao watahakikisha wanamsambaza haraka sana. Hatuko salama na hatutakuwa salama. Hii ni vita ngumu sana na yawezekana wengi wetu tusifanikiwe kufika mwisho lakini vyovyote vile itakavyokuwa lazima tuhakikishe mabeberu hawashindi na hili litakuwa ni fundisho kwao kuacha kuichezea Tanzania.”

“Mathew nini mawazo yako? Tunatokaje hapa tulipofika kwenda mbele? Aliuliza Gosu Gosu.

“Kitu cha kwanza ni kuweka mikakati namna ya kupambana kuhakikisha mipango tuliyoisikia haifanikiwi. Haya si mapambano rahisi hata kidogo. Ninamfahamu vizuri Israel Maungwana, ni mtu mkatili na hatari. Uwepo wake katika jambo hili ni ishara kuwa mapambano haya

yatakuwa magumu mno. Mabeberu walio nyuma ya makundi haya tuliyoyafahamu ambayo yanawania uongozi wa nchi hii lazima wamejiandaa kikamilifu kuhakikisha hakutokei mkwamo wa aina yoyote ile ndiyo maana wamekuwa wakichunguzana kujua kila kinachofanywa na kundi lingine.” Alinyamaza na kumgeukia Gosu Gosu.

“Gosu Gosu walete watu wengine wote humu ndani”

“Regina na Lucy pia? Aliuliza Gosu Gosu.

“Ndiyo. Wote nawahitaji” alijibu Mathew na Gosu Gosu akatoka.

“Mathew wewe ndiye kiongozi hapa. Ninahitaji kusikia kauli yako baada ya kuwaeleza kila kitu kinachoendelea. Je nimekubaliwa kujiunga nanyi?” aliuliza Julius.

“Maelezo uliyotupa ni mazito na yamenishawishi nikubali kukujumuisha katika

timu yetu. Tuwapo katika misheni hufanya kazi usiku na mchana. Kanuni yetu kuu ni ukweli. Nitakapogundua u msaliti au kuna mambo umetuficha nakuhakikishia nitazamisha risasi katika kichwa chako. Unapokuwa hapa pamoja nasi utafuata maelekezo yote utakayopewa. Kuna mtu mmoja tu anayetoa maelekezo humu ndani ambaye ni mimi. Umenielewa Julius? Mathew aliuliza.

“Nimekuelewa Mathew na ninakushukuru mno kwa kunikubali na kunikaribisha katika timu yenu. Nimeyakubali masharti yenu na ninakuhakikishia kuwa hakuna nilichokificha. Kila kitu nimewaeleza.”

“Good. Welcome to the team.” Alisema Mathew.

Mlango wa chumba ulifunguliwa wakaingia Ambola, Regina, Thomas Ngalula na Jombaa. Regina mwili ulimtetemeka baada ya

kumkuta Julius ndani ya kile chumba. Hakutegemea. Baada ya sekunde chache ilisikika sauti ya mwanamke akipiga kelele. Mathew alipiga hatua kutaka kutoka mle ndani kwenda kuangalia kilichotokea lakini mara akaingia Gosu Gosu akiwa amembeba begani Lucy.

“Hakutaka kuja nimelazimika kutumia nguvu.” Alisema Gosu Gosu. Baada ya kushushwa chini Lucy aligeuka kwa kasi akamsukuma Gosu

Gosu na kutaka kutoka nje ya kile chumba. Gosu Gosu alipepesuka kidogo halafu akawahi kuudaka mkono wa Lucy akamvuta na kumnasa kofi zito lililompeleka Lucy chini. Gavana alifumba macho baada ya mke wake kuanguka kwa kishindo. Gosu Gosu alimfuata pale chini akamuinua. Alitaka kumuongeza kipigo lakini Mathew aliwahi akaudaka mkono.

“Imetosha.”

“Mathew hawa wanawake wanapaswa kufundishwa adabu ili wafahamu hapa wako mahali gani” alisema Gosu Gosu.

“Jamani nimewaiteni hapa nyote kuna jambo la muhimu sana ambalo mnapaswa kulifahamu.” Alisema Mathew na kabla hajasema chochote alifanya utambulisho kwa kila mmoja aliyekuwemo mle ndani. Baada ya utambulisho ule Mathew alieleza kwa ufupi kile kilichotokea Arusha na

wakafanikiwa kumuokoa Regina. Alieleza kilichoendelea hadi walipofika Dar es salaam. Alieleza kila kitu tangu alivyoonana na Gavana hadi walivyogundua Regina ana simu ambayo amekuwa akitumia kuwasiliana na Lucy.

“Nimewapa maelezo haya kwa sababu ninataka wote tuwe katika ukurasa mmoja” alisema Mathew na kueleza kila kitu kilichotokea hadi Julius alivyofika pale.

“Ninaweza kusema ni kwa maongozi ya Mungu Julius amekuja hapa. Ametueleza kila kitu kuhusu ninyi wawili Lucy na Regina. Tulipowahoji kuna mambo hamkusema ukweli lakini Julius tayari ametueleza kila kitu. Sasa tunawafahamu ninyi ni akina nani pamoja na shughuli zenu.”

“Mathew anasema kweli. Nimewaeleza kila kitu kuhusu sisi na kile tunachokifanya. Huu si muda wa kuficha mambo. Tunahitaji kuungana

na watu kama hawa ili kufanikisha mipango yetu tuliyokwisha ianza.” alisema Julius.

“Lucy na Regina kile kipindi cha kutesana ili kueleza ukweli kimekwisha. Ninalifungua dirisha lingine kwenu kama mko tayari kujiunga nasi katika mapambano ya kuikomboa nchi yetu. Hamlazimishwi. Kila mmoja ana hiyari ya kukubali kuungana nasi au kukataa. Ambaye hatakuwa tayari

hatutamfanya chochote we'll let her go" alisema Mathew.

"Lucy na Regina siwalazimishi lakini ninawaomba mkubali kujiunga na timu hii ambayo ndiyo itafanikisha kile ambacho tumekuwa tunakifanya kwa siri. Hawa ni watu wenye uzoefu mkubwa zaidi lakini wao pia walikuwa wanakifanya kile ambacho sisi tunakifanya isipokuwa hawakuwa wanalifahamu jambo hili kwa upana wake. Kwa sasa baada

ya kuwaeleza kila kitu hakuna haja ya kuwa na makundi mawili ambayo misheni yake ni moja. Tuungane pamoja kuikomboa nchi yetu" alisema Julius.

"I'm ready" alisema Regina kwa sauti ya chini.

"Toa sauti! Alifoka Gosu Gosu.

"I'm ready" alirudia Regina.

"Good. Lucy we unasemaje? Aliuliza Mathew.

“Naweza kupewa dakika mbili kuzungumza na mume wangu kwanza? Aliomba Lucy.

“Hakuna tatizo. Ninakupa dakika tano kama kuna kitu chochote unataka kumwelexa itumie nafasi hiyo” alisema Mathew.

“Hapana” Gavana aligoma.

“Kama kuna kitu chochote anataka kuzungumza nami basi akiseme mbele yenu.”

“Mzee kuna mengi yametokea hivyo tunawapa

dakika chache za kuzungumza pengine mnaweza kuweka mambo sawa ili tuendelee na misheni yetu”

“Mathew ahsante sana kwa hilo unalotaka kulifanya lakini mimi ninataka azungumze mbele yetu sote kama analo la kuniambia bila kujali kama ni suala la ndoa. Huyu ni mke wangu kwa zaidi ya miaka thelathini hivi sasa na tumeishi muda huo wote kwa amani na upendo mkubwa. Sijawahi kumficha jambo na niliamini

hata yeye hajawahi kunificha jambo lakini kwa yale niliyoyasikia usiku huu ni mshituko mkubwa ndiyo maana nilipoteza fahamu nilipomuona hapa. Tusipoteze muda Lucy kama una jambo la kuniambia wakati ni huu." Alisisitiza Gavana. Msimamo wake haukuyumba.

"Lucy umemsikia Gavana alichokisema. Kama una jambo ambalo unataka kumweleza fanya hivyo sasa ili tuendelee na mengine." Alisema Mathew.

Lucy aliinuka akapiga hatua tatu halafu akapiga magoti mbele ya mume wake. Alimtazama usoni. Michirizi ya machozi ilionekana machoni pake. Sura yake ilionesha majuto makubwa. Gavana naye alionekana kumshangaa mke wake kana kwamba ni mara ya kwanza anamuona.

“Jackson” alisema Lucy na kunyamaza akafuta machozi halafu akasema.

“Sifahamu nianzie wapi lakini naamini hawa vijana

tayari wamekueleza kila kitu.” Alinyamaza tena akafuta machozi.

“Kitu gani kinakuliza Lucy? Aliuliza Gavana.

“Nimekufanyia mambo mabaya sana ambayo sijui nitafanya nini kuyafuta katika moyo wako. Sitaki kupoteza muda kuyarudia hapa kwani tayari unayafahamu. Kwa yale yote niliyokukosea naomba unisamehe. Nipe nafasi nyingine. Nitakuwa mke mwema na mtiifu. Sintakuficha

kitu chochote tena. Kuanzia sasa sintafanya tena kazi ile niliyokuwa naifanya. Please forgive me Jackson” alisema Lucy na kuinama chini akaishika miguu ya Gavana.

“Nisamehe Jackson” alilia Lucy. Chumba chote kilikuwa kimya kabisa. Kilichokuwa kinaendelea mle ndani kilimsisimua kila mtu.

“Gavana.” Aliita Mathew na kukohoa kidogo. Gavana alishindwa kuzungumza akabaki anamtazama Mathew.

“Msamaha upo kwa sababu dhambi au makosa yapo. Msamaha ni maalum kwa wakosaji. Msamaha ni roho ya Mungu kwani asili ya msamaha ni Mungu mwenyewe. Roho ya kutokuomba au kutokutoa msamaha ni ya Shetani. Alipomuasi Mungu, Shetani aliendelea kuutetea uovu wake na kufanya vita na Mungu. Mtanisamehe kama nitachukua muda wenu lakini fahamuni asiyesamehe hawezi

kuomba msamaha na asiyeomba msamaha hawezi kusamehe. Mke wako amekukosea. Amelifahamu kosa lake amekiri na kuomba msamaha. Hatukulazimishi kumsamehe ila kama utaona inafaa basi msamehe" alisema Mathew. Gavana alimtazama Mathew kwa muda kidogo akapeleka mkono wake machoni akafuta machozi.

"Mwanamke huyu nimeishi naye kwa zaidi ya miaka thelathini. Mungu pekee ni

shahidi kwa namna ninavyompenda lakini leo amediriki kuniuza kwa wenzake wakanitesa sana. Mathew siwezi kusema hapa kuwa nimemsamehe. Naomba suala hili tuliweke pembeni kwanza tujielekeze katika kile kinachoendelea hivi sasa. Lucy inuka tutazungumza wakati mwingine lakini kwa sasa ni masuala muhimu kwa nchi" alisema Gavana na kuinuka kutoka mahali alipokuwa amekaa na kwenda kukaa

sehemu nyingine akamuaca Lucy akilia. Mathew alimtaka Gavana watoke nje wakazungumze.

“Gavana tunahitaji kwenda kuonana na Kelvin. Mtu pekee anayefahamu mahali alipo ni mkeo Lucy. Ninakuomba ujaribu kumshawishi ili akubali kutupeleka huko aliko Kelvin. Najua ni jambo gumu kwa kuwa bado una hasira lakini kwa manufaa ya operesheni yetu naomba ufanye hivyo. Jishushe ili Lucy

akubali kutupeleka alipo Kelvin. Naamini hata wewe mwenyewe una hamu sana ya kutaka kuonana na mwanao. Hakuna mwingine wa kutupeleka aliko Kelvin zaidi ya Lucy" alisema Mathew.

"Mathew kila ninapokumbuka mateso niliyoyapata leo kutoka kwa wale mabazazi ninapandwa na hasira sana"

"Ninafahamu mzee lakini kwa sasa ni Lucy pekee aliyeshika mpini. Nilikuahidi

kukusaidia kupata ukweli kuhusu mwanao na tayari ukweli umejulikana Kelvin yuko hai. Ninataka kuonana naye nione namna tunavyoweza kushirkiana naye katika operesheni hii" alisema Mathew. Gavana alifikiri kwa muda halafu akasema.

"Sawa nitajaribu kuzungumza naye"

Mathew aliingia ndani akamuinua Lucy akamtoa nje ya chumba aliko Gavana akawaacha peke yao

wazungumze. Gavana alimtazama mke wake kwa sekunde chache halafu akasema.

“Lucy nisamehe kwa maneno yale makali niliyoyatoa mle ndani. Najua unataka tuzungumze lakini mambo haya ni makubwa na tunahitaji muda wa kutosha. Ninakuahidi tutapata nafasi ya kutosha tutazungumza na kuyaweka sawa. Nikisema nimekusamehe hapa nitakuwa nakudanganya kwani nahitaji

kufahamu mambo haya kwa ndani zaidi. Kwa kuwa umekiri mwenyewe kwamba hakuna siri tena ninataka unithibitishie hilo kwa kunipeleka mahali alipo Kelvin. Nimeambiwa ni wewe pekee unayefahamu mahali alipo hivyo nahitaji unipeleke mahali hapo usiku huu.” alisema Gavana. Lilionekana ni jambo gumu kwa Lucy. Baada ya kufikiri kwa muda akasema.

“Sawa nitakupeleka *but only you*” alisema Lucy.

“Nitaambatana na Mathew Mulumbi, Julius, Ruby na Gosu Gosu” alisema Gavana. Lucy alifikiri tena kwa muda halafu akasema.

“Sawa nitawapeleka”

Gavana aliingia ndani akamjulisha Mathew kuwa Lucy amekubali kuwapeleka mahali aliko Kelvin. Mathew aliwaita nje Julius,Ruby na Gosu Gosu, akawafahamisha kuhusu safari ile. Aliwataka wengine wote wapumzike na wasubiri maelekezo zaidi

atakaporejea. Hawakupoteza muda waliingia garini wakaondoka kuelekea mahali aliko Kelvin.

****

Gari moja lilikaribia geti la jumba la kifahari la mwenyekti wa chama cha Ukombozi wa Afrika Israel Maungwana. Mmoja wa walinzi alijitokeza na kulisimamisha. Dereva alishusha kioo na kutoa kadi Fulani akampatia yule mlinzi ambaye aliipitisha katika mashine ndogo mithili ya simu

aliyokuwa ameishika mkononi. Taarifa za dereva yule zilionekana katika kile kifaa. Wakati mlinzi yule akikagua taarifa za dereva, walinzi wengine watatu walijitokeza na kulikagua lile gari kwa vifaa maalum ili kujiridhisha halina hatari yoyote. Baada ya kuridhika na ukaguzi ule, geti lilifunguliwa dereva akaruhusiwa kuendelea na safari. Gari lile liliingia ndani na kwenda kusimama nje sehemu ya chini. Mlango

ilifunguliwa na watu watatu wakashuka. Dereva aliwaongoza watu wale hadi katika mlango mkubwa wa kuingilia ndani akabonyeza kengele. Baada ya muda mfupi mlango ulifunguliwa akajitokeza Israel Maungwana akawakaribisha ndani wageni wake. Moja kwa moja aliwapeleka katika ofisi yake.

“Karibuni sana. Hapa ni nyumbani kwangu.” Alisema Israel.

“Utatusamehe kwa kuchelewa. Kikao na mwenyekiti wa tume ya uchaguzi kilikuwa kirefu sana lakini kila kitu tumekimaliza. Kesho tutaanza rasmi kazi.” Alisema mmoja wa wale jamaa.

“Hiyo ni taarifa njema sana. Nimetaka mpite hapa baada ya kutoka katika kikao nina mazungumzo muhimu sana nanyi. Kuna tatizo dogo limetokea usiku huu hivyo nitaomba msaada wenu katika kulishughulikia.”

“Tumekuja kufanya kazi. Kama ipo kazi ya kufanya tupe maelekezo”

“Ahsante sana.” Israel aliwaeleza kila kitu kuhusu Julius.

“Kwa kuwa hakuna mtu wa karibu anayeweza kuongoza idara hiyo ya SNSA kwa sasa, nimewapendekeza ninyi mtusaidie kuiongoza kwa muda hadi pale atakapopatikana mtu maalum. Mtatusaidia kwa kipindi hiki cha kampeni hadi pale misheni

itakapokamilika ndipo kazi yenu itakapokamilika.” Alisema Israel wakaendelea kujadiliana kwa muda kuhusiana na majukumu yao mengine na baada ya muda Israel akasema.

“Kuna jambo lingine ambalo nataka mtusaidie mkiwa hapo SNSA. Nataka mtusaidie kumsaka mtu huyu” alisema Israel na kuwaonesha wale jamaa picha katika kompyuta yake.

“Hiki ni kirusi kingine ambacho tunatakiwa kuhakikisha tunakimaliza ndani ya kipindi kifupi sana.” Alisema Israel.

“Ni nani huyu mtu?” aliuliza mmoja wa wale jamaa.

“Anaitwa Mathew Mulumbi. Amewahi kufanya kazi katika shirika la ujasusi Tanzania. Ni mtu hatari sana ambaye kama asipodhibitiwa mapema anaweza akaleta madhara makubwa kwetu. Tayari amefahamu mipango

yetu. Yeye na kundi lake wamejipanga kuhakikisha haifanikiwi na tayari kuna hatua wamekwisha piga. Hawatakiwi kwenda zaidi ya walipofika. SNSA wana kila kitu kinachoweza kutusaidia kuwapata hawa watu kwa haraka hivyo naomba kazi hizo mbili kumsaka Julius na Mathew Mulumbi kiwe ndicho kipaumbele chenu" alisema Israel.

Mikakati mbali mbali ilipangwa usiku ule namna

wale jamaa watakavyofanikisha kupatikana kwa akina Mathew kwa kutumia idara ya SNSA. Kisha kubaliana namna ya kufanya jamaa wale waliondoka kwenda kupumzika kabla ya asubuhi kuanza kazi SNSA.

****

Akina Mathew waliikaribia nyumba yenye mfumo maalum wa kisasa kabisa wa ulinzi ambao ulimuwezesha mtu aliyeko ndani kutambua kwa haraka mvamizi yeyote na kuchukua hatua ikiwamo kumuua kwa kutumia silaha maalum za kielektroniki zilizofichwa mahali pa siri juu ya nyumba ile. Kamera kumi na mbili za siri zilionesha kila kilichokuwa kinafanyika

kulizunguka jumba lile. Mlango wa kuingilia ndani ya nyumba ile ulikuwa imara wenye uwezo wa kuhimili milipuko. Madirisha yake yalitengenezwa kwa teknolojia ya aina yake ili kutosababisha madhara yoyote kwa watu waliomo ndani pale unapotokea mlipuko wa aina yoyote. Hii ndiyo nyumba aliyokuwa akiishi Kelvin tangu alipotoweka.

Gari la akina Mathew liliikaribia nyumba ile na taa

tatu kubwa ziliwaka na kulifanya eneo lile lionekane kama mchana halafu zikazima. Baada ya kuufikia mstari Fulani mweupe Lucy alimtaka Gosu Gosu aliyekuwa dereva asimamishe gari. Alifungua mlango akashuka akatembea hadi getini ambako alipitisha kiganja cha mkono wa kulia katika kisanduku Fulani kikawaka taa ya kijani halafu kikajifungua na namba zikajitokeza. Alibonyeza namba kadhaa na kukifunga kile

kisanduku halafu akarejea garini akamtaka Gosu Gosu aendeshe gari. Mita chache kabla ya kulifikia geti, lilifunguka wakaingia ndani kisha likajifunga. Mbwa wawili wakubwa walijitokeza. Lucy alishuka garini akawapa maelekezo mbwa wale watiifu wakakimbia kurejea katika nyumba yao. Aliwataka akina Mathew washuke garini kisha wakaelekea katika mlango ule wa aina yake. Alibonyeza namba Fulani na mlango

ukafunguka wakaingia katika chumba kimoja kilichokuwa na rangi nyeupe. Hakukuwa na mlango wowote ndani ya chumba kile. Walisimama katikati ya chumba baada ya sekunde kadhaa ikalia kengele.

“Kama kuna mtu ana silaha aitoe aiweke katika lile kasiki” alisema Lucy huku akielekea katika kasiki akalifungua. Mathew na Gosu Gosu waliokuwa na bastola walizitoa wakaziweka katika kasiki wakarudi kusimama kati kati

ya chumba kile. Ulitokea mwangaza wa bluu halafu ukatokea tena mwangaza mwekundu na mara sehemu ya ukuta ikajifungua wakaingia ndani.

“Dah !” Gosu Gosu alishangaa kwa ulinzi ule.

Waliingia katika chumba kingine ambako walipita katika mtambo uliotoa mvuke wa dawa kwa ajili ya kuhakikisha kila anayeingia ndani hajabeba vimelea vya magonjwa.

Baada ya hatua ile ndipo walipokwenda sebuleni. Mara tu walipoketi sebuleni alitokea mtu aliyewafanya watu wote waliokuwa wamekaa wasimame. Gavana alitetemeka kwa mshituko alioupata baada ya kumuona mwanae Kelvin ambaye kila mtu aliamini amefariki dunia.

“Baba” alisema Kelvin ambaye naye alipatwa na mshituko mkubwa.

“Kelvin” alisema Gavana na kushindwa kuyazuia machozi

kumtoka. Kelvin alipiga hatua za haraka haraka akamkumbatia baba yake. Lucy alisimama pembeni akiwatazama huku akibubujikwa machozi.

“Nimelia machozi mengi sana kwa ajili yako Kelvin. Nimemuomba Mungu sana aniangazie nifahamu mahali ulipo. Kila siku ninaamka saa tisa usiku nikimlilia Mungu akulinde kama uko hai na siku moja tukutane tena. Leo Mungu amejibu kilio changu.

Nimekutana nawe tena mwanangu” alisema Gavana huku akibubujikwa na machozi ya furaha. Kelvin alipiga magoti.

“Baba naomba unisamehe sana kwa mateso yote niliyokusababishia. Haikuwa nia yangu kufanya hivi nilivyofanya lakini…” Kelvin alisema huku machozi yakiendelea kumtoka. Gavana alimuinua.

“Kelvin huna haja ya kuomba msamaha. Yote

yaliyotokea, maumivu yote niliyokuwa nayo yamemezwa na furaha kubwa niliyoipata baada ya kuiona tena sura yako.” Alisema Gavana na kumkubatia tena mwanae.

“Baba kabla hatujazungumza chochote hadi umefika hapa naamini tayari umefahamu kila kitu. Ninakuomba msamehe mama kwa kukuficha ukweli kuhusu jambo hili. Ni yeye pekee anayefahamu mahali nilipo na kila siku ajapo hapa amekuwa

akimwaga machozi akijiuliza nini kitatokea siku utakapogundua jambo hili. Sifahamu nini kimetokea lakini naamini lazima upo mgogoro mkubwa. Nawaomba wazee wangu kama kuna mgogoro wowote uliotokea kwa sababu ya hili suala langu muumalize kwani ninayepaswa kulaumiwa ni mimi.” Alisema Kelvin.

“Kelvin mambo yote yamekwisha. Hakuna mgogoro tena” alisema Gavana.

“Nashukuru sana baba” alisema Kelvin kisha akawaleta karibu baba na mama yake wakakumbatiana kwa pamoja.

“Kelvin tumejisahau kwa furaha iliyopitiliza baada ya kuonana. Kuna wenzetu tumeambatana nao ambao nimesahau kuwatambulisha. Wa kwanza ni Mathew Mulumbi.”

“Hili jina nimewahi kulisikia katika mambo ya biashara” alisema Kelvin.

“Ndiyo. Ni mmoja wa wawekezaji wakubwa hapa nchini. Ni mmoja wa mabilionea wazawa.”

“Karibu sana kaka” alisema Kelvin.

“Tunaye pia mtu anaitwa Gosu Gosu. Tunaye pia Ruby. Wa mwisho tuliyeongozana naye ni Julius huyu naamini unamfahamu.”

“Julius ninamsikia tu. Ni mara ya kwanza mimi naye kuonana ana kwa ana.” Alisema Kelvin. Kwa furaha

aliyokuwa nayo Kelvin alileta chupa za mvinyo akaziweka mezani.

“Ahsante sana Kelvin kwa makaribisho haya mazuri lakini kabla ya kuburudika kwa vinywaji tunapaswa kumaliza kwanza kile kilichotuleta mahali hapa.” Alisema Mathew.

“Mathew hatuwezi kutumia muda kidogo tukajipongeza kwa jambo hili kubwa? Kwangu ni kama muujiza

kuonana tena na mwanangu” alisema Gavana.

“Mzee ninafahamu furaha uliyonayo lakini utapata muda mrefu wa kukaa na familia yako mkazungumza mambo mengi. Kwa sasa tumalize kwanza kile kilichotuleta hapa.” Alisisitiza Mathew. Wakati Mathew akisisitiza tayari Gosu Gosu alikuwa anamalizia mvinyo aliomimina katika glasi.

“Sawa Mathew.” Alisema Gavana na kumtazama Kelvin.

“Kelvin tumekuja hapa kwa mambo mawili.Moja ni kukutana nawe na pili ni kuhusiana na kile kinachoendelea hapa nchini” alisema Gavana na kumpa nafasi Mathew ambaye alianza kumweleza Kelvin kila kitu kuhusu tukio la Regina kutaka kuuawa jijini Arusha. Alieleza kila kitu hadi walivyokutana na Julius na mambo yote mazito aliyowaeleza. Baada ya Mathew kumaliza kutoa

maelezo,Lucy naye alinyoosha mkono na kusema.

“Ninaomba mnipe nafasi niseme neno kwa dakika chache” alinyamaza kidogo.

“Endelea” alisema Mathew.

“Kama alivyosema Julius, nimekuwa mfanyakazi wa shirika la ujasusi Tanzania kwa muda mrefu.Nimejitahidi sana kumficha mume wangu jambo hilo lakini Kelvin anafahamu kila kitu. Mimi na Sophia Mnambara ni marafiki wakubwa na niliutumia urafiki

huo kumsaidia Kelvin kuingia SNSA akiwa katika kitengo cha majasusi wa siri. Ni mimi niliyempa Sophia wazo la kuanzisha kampuni ya Tarmo na Kelvin ndiye aliyekuwa mpelelezi wa kwanza kufanya kazi na kampuni hiyo hadi pale maisha yake yalipokuwa hatarini tukatengeneza lile tukio na nikamleta hapa kujificha. Nilitaka niweke sawa jambo hilo ila mengi atawaeleza Kelvin mwenyewe” alisema Lucy.

“Mama anayosema ni kweli kabisa. Sitaki kurudia nataka kuanzia pale alipoishia. Nikiwa nafanya kazi SNSA na wakati huo huo nikifanya kazi za Tarmo yaani kuichunguza SNSA kama walihusika katika mauaji ya baba na kaka wa Sophia Mnambara, uliibuka utata wa kifo cha Rais Mstaafu Malaki Mnambara. Tetesi zilidai yuko hai. Nililazimika kufanya uchunguzi wa kina kubaini ukweli kama kweli Malaki alifariki dunia au yuko

hai kama tetesi zilivyodai. Nilishirikiana na Faraji Dilele ambaye alikuwa mkurugenzi wa SNSA wakati ule. Haikuwa kazi rahisi lakini niliupata ukweli. Malaki Mnambara yupo hai. Hakufariki dunia kama inavyodaiwa. Kifo chake kilitengenezwa kwa sababu maalum kumnusuru na tuhuma mbali mbali zilizokuwa zinamkabili. Kwa sasa Malaki anatumia jina la Benard Timothy. Ana makazi ya kudumu katika nchi tano za

Ulaya na Amerika. Malaki amekuwa akitumiwa na mabeberu kufanikisha mipango yao ya kutaka kuingia nchini Tanzania kuchuma rasilimali zilizopo hasa madini hivyo alianzisha chama cha Ukombozi wa Afrika. Mipango yote inayofanywa na chama hiki na mtandao alioutengeneza tayari mmeelezwa na Julius. Mimi nikishirikiana na mama pamoja na hawa akina Julius ambao sijawahi kuonana nao

hata mmoja wao, tuna mipango ya siri kuhakikisha mipango yote ya mabeberu haifanikiwi. Imekuwa vyema na ninyi mmetokea wakati mipango yetu ikiendelea.” alinyamaza Kelvin.

“Kelvin ahsante kwa maelezo yako. Nakupongeza kwa jambo kubwa ulilolifanya la kumchunguza Malaki Mnambara na kugundua yuko hai. Ulihatarisha maisha yako lakini kwa manufaa makubwa ya nchi.Hongera sana.”

“Ahsante Mathew.”

“Kelvin, baada ya kuufahamu ukweli wote sisi tumeamua kuunganisha nguvu na kuwa timu moja ili tushirikiane katika misheni ya kuvuruga mipango yote ya mabeberu dhidi ya nchi yetu. Nataka kufahamu namna mlivyojipanga kuvuruga njama zote za uchaguzi mkuu.” Alisema Mathew.

“Ni kweli mimi na wenzangu tumeazimia kuhakikisha mipango yote ya

mabeberu dhidi ya nchi yetu haifanikiwi lakini mpaka sasa bado hatuna mpango wowote mahsusi. Tunachokifanya tumeelekeza macho na masikio yetu katika makundi haya yanayopambana kutwaa uongozi wa Tanzania ili tuifahamu mipango yao. Baada ya kuifahamu mipango yao ndipo tutaamua nini tufanye. Bado tuko katika hatua za awali za kukusanya taarifa namna makundi haya yalivyojiandaa kuvuruga

uchaguzi wetu.” alisema Kelvin.

“Awali niliwaambia wengine kwamba, nchi yetu ni kama Swala mnono mbele ya kundi la Mbwa mwitu wenye njaa kali sana. Swala mnono ni utajiri wetu na Mbwa mwitu ni mabeberu wenye njaa wanaohitaji kuzipata rasilimali zetu. Ni wajibu wetu kuhakikisha tunapambana kulinda nchi yetu,kulinda uhuru wetu na kulinda rasilimali zetu. Wakati pekee

wa kufanya hayo ni sasa. Mabeberu hawa wamejipanga vilivyo. Hawataki kushindwa. Mipango yao haijaanza jana wala juzi. Wameanza kujiandaa muda mrefu. Kuwabomoa kwa haraka si jambo jepesi kwani tayari wamekwisha penyeza mizizi yao katika serikali. Wameigawa serikali vipande vipande na kwa sasa hata zile taasisi nyeti kabisa ambazo zinahusika na mambo muhimu kama uchaguzi ziko katika mikono ya

mabeberu. Tume ya uchaguzi ni chombo muhimu sana ambacho kazi yake ni kuandaa na kuhakikisha uchaguzi mkuu unafanyika kwa uhuru na haki. Chombo hiki muhimu kabisa tayari kiko mikononi mwa mabeberu. Tayari wameletwa wataalamu kwa ajili ya kuuvuruga mfumo wa tume ya uchaguzi na kukipa ushindi chama cha ukombozi wa Afrika. Taasisi nyingine muhimu kama jeshi la polisi tayari viongozi wake wako

katika mikono ya mabeberu. SNSA idara nyeti kabisa imegeuzwa majukumu na sasa inatumika kuhakikisha mipango ya mabeberu inafanikiwa. Kubwa kuliko yote, Rais anayemaliza muda wake Dkt Nehemia ambaye ni zao la Rais mstaafu Malaki Mnambara, ndiye kinara wa njama hizi za kuvuruga uchaguzi mkuu na kuhakikisha mabeberu wanashinda. Wameahidiwa utajiri mkubwa ambao utawafanya waishi

kama wako peponi.” Alisema Mathew na kuwatazama watu wote mle chumbani ambao walikuwa kimya wakimsikiliza.

“Sitaki kuwavunja nguvu ndugu zangu lakini mlima tunaoupanda ni mrefu sana na yawezekana tusiweze kufika kileleni kabla ya uchaguzi mkuu kufanyika.”

“Mathew yuko sahihi. Hawa jamaa wamejipanga kikamilifu hasa kundi hili la Tanzania mpya ambalo limepiga hatua kubwa katika kuhakikisha

wanashinda uchaguzi.” Alisema Julius.

“Sasa nini kifanyike vijana? Hatuwezi kuwaacha wakavuruga uchaguzi wetu.Hatuwezi kuwaacha mabeberu wakatalawa nchi yetu. We must do something !” alisema Gavana.

“Mpaka sasa tumeyafahamu makundi kadhaa ambayo yamejipanga kushinda uchaguzi mkuu. Hatuna muda wa kutosha kuyashughulikia makundi yote

kwa sababu tayari yamepiga hatua kubwa katika kufanikisha mipango yao. Kuna jambo moja tu ambalo ninadhani linapaswa kufanyika ili kuzima mipango ya mabeberu” alisema Mathew na kunyamaza.

“Jambo gani hilo Mathew? Aliuliza Gosu Gosu.

“Kuzuia uchaguzi mkuu usifanyike katika tarehe iliyopangwa.” Alijibu na kunyamaza kidogo akawatazama wenzake.

“Tayari fedha nyingi zimetumika kuandaa uchaguzi huo. Kuzuia uchaguzi ni kuliingiza taifa katika hasara kubwa. Hata hivyo ni namna gani tunaweza kuzuia uchaguzi huo usifanyike? Aliuliza Kelvin.

“Kuna siri ambayo mnatakiwa kuifahamu. Uchaguzi huu unafadhiliwa na mataifa ya nje kwa asilimia tisini na saba. Fedha zetu ni asilimia tatu tu.” alisema Gavana.

“Ahsante Gavana kwa kutupa picha hiyo. Lazima tujiulize kwa nini wametoa fedha hizo zote kugharamia uchaguzi wetu mkuu? Katika nchi zao hakuna mambo ya maendeleo yanayohitaji fedha hadi wazitupe huku kwetu?” Mathew aliuliza.

“Ufadhili huu mkubwa si bure. Lazima kuna kitu wanatarajia kukipata baada ya uchaguzi.” Alijibu Gavana.

“Tunao utajiri mkubwa mno wa rasilimali. Kwa nini

tunashindwa kugharamia uchaguzi wetu wenyewe? Hii ni aibu kubwa. Jambo hili lazima lifike mwisho. Wakati mwingine hawa mabeberu wanatuchezea kwa sababu tunataka wenyewe kuchezewa. Tukiamua kusimama imara na kusimamia rasilimali zetu hakuna beberu atakayeleta pua yake hapa nchini.” Mathew alizungumza kwa uchungu mkubwa.

“Maamuzi mazito ya kuikomboa nchi yetu kutoka

katika mikono ya mabeberu lazima yafanyike katika chumba hiki. Kama hatutaweza kuamua usiku huu, tutakuwa tumeikabidhi nchi yetu katika mikono ya mabeberu. Lazima tufanye maamuzi magumu mno usiku huu kwa maslahi makubwa ya nchi yetu" alisema Mathew.

"Mathew ninakubaliana nawe kabisa. Usiku huu uwe ni wa maamuzi makubwa ya kuinusuru nchi yetu isiangukie

katika mikono ya mabeberu.” Alisema Gavana.

“Sote tuliomo humu kila mmoja ni mzalendo wa kweli na dhumuni letu ni moja tu kuinusuru nchi yetu isiangukie katika mikono ya mabeberu. Nikiitazama sura ya kila mmoja humu ndani yuko tayari kwa mapambano” alisema Kelvin.

“Mathew tupe mwongozo. Nini tufanye? Alisema Gosu Gosu.

“Kuna mambo mawili ambayo nafikiria yafanyike na nitaomba mniunge mkono. Jambo la kwanza ni kuhakikisha uchaguzi mkuu haufanyiki katika tarehe iliyopangwa na badala yake usogezwe mbele ili kutupa nafasi ya kujiandaa kikamilifu kuvuruga mipango yote ya makundi ya mabeberu. Swali ni namna gani tunaweza kuzuia uchaguzi mkuu usifanyike katika tarehe iliyopangwa? Tarehe ya

uchaguzi ikishatangazwa kuna namna moja tu inayoweza kupelekea tarehe hiyo ikaahirishwa nayo ni endapo moja wa wagombea urais atafariki dunia. Mpango wangu ni kuua wagombea urais wa makundi yote yanayofadhiliwa na mabeberu.”Mathew alinyamaza kidogo halafu akawatazama wenzake ambao nyuso zao zilionesha mshangao.

“Kulizungumza jambo hili ni rahisi lakini utekelezaji wake

ni mgumu. Lazima umwagikaji mkubwa wa damu utokee kwa sababu wagombea hawa wamepewa ulinzi tangu siku walipoteuliwa na tume ya uchaguzi hivyo ili kuwamaliza itatulazimu kuwaondoa na walinzi wao pia" alisema Mathew.

"Hili ni jambo jipya ambalo halikuwepo kichwani mwangu" alisema Gavana.

"Mathew nimeelewa lengo lako la kutaka kuua baadhi ya wagombea urais ili tupate

muda wa kujipanga vyema kuvuruga mipango yote ya mabeberu.Kama ni hivyo kwa nini tusiue mgombea mmoja ili uchaguzi uahirishwe kwa siku 90? Naamini katika siku hizo 90 tayari tutakuwa tumejipanga vya kutosha.” Alishauri Julius.

“Nilisema haya ni maamuzi magumu sana ya kuhakikisha tunawaondoa mabeberu na vibaraka wao hapa nchini. Lazima tusafishe nchi. Tukimuondoa mmoja na

wengine wakibaki wataendelea kugombea. Hawa wote hawana sifa za kuwa viongozi wetu.Wote ni vibaraka wa mabeberu. Hakuna kuwaonea huruma”

“Mathew sidhani kama hili ni wazo jema” alisema Lucy.

“Kama yupo mwingine mwenye wazo mbadala alilete ili tuone kama linafaa” alisema Mathew. Watu wote walibaki kimya.

“Hakuna mwenye wazo mbadala. Hiki

ninachowaambia ndicho pekee tunachoweza kukifanya ili tupate muda wa kutosha kujipanga kuwafurusha mabeberu wote na vibaraka wao”

“Lakini Mathew sisi ni wakombozi na si wauaji” alisema Kelvin.

“Hii ni vita ya kuikomboa nchi na kulinda rasilimali zetu.Hili si jambo la mzaha hata kidogo. Uhuru wetu, rasilimali zetu lazima vilindwe kwa gharama zozote zile hata

kama ni kwa kumwaga damu. Hakuna kumuonea huruma mtu yeyote kwani wao hawaoni huruma kutaka kuchezea haki ya watanzania kuchagua kiongozi wamtakaye. Ndugu zangu siwalazimishi mkubaliane nami katika jambo hili kwani hata kama nitabaki peke yangu hicho ndicho kitu pekee nitakachokifanya.” Alisema Mathew.

“Mathew chochote kile utakachoamua kukifanya niko

nyuma yako” alisema Gosu Gosu.

“Me too” alisema Ruby.

“Mimi pia ninaunga mkono” aliongeza Gavana.

“Nami nakubaliana na mpango huo” alisema Julius.

“Mpango huo utatuingiza katika matatizo makubwa sana jamani” alisema Kelvin.

“Matatizo hatuwezi kuyaepuka. Lazima tukabaliane nayo. Niwaulize swali. Kipi bora kama watu

kumi wataingia katika matatizo au watu milioni sitini kuteseka kwa kukosa huduma bora za afya, maji na elimu wakati rasilimali zao zikisombwa na watu wachache? Nadhani ni bora wachache wakaingia katika matatizo kuliko kuacha watu milioni sitini na zaidi wakaingia katika tatizo la umasikini mkubwa. Kwa yeyote ambaye ni mwoga wa kuingia katika matatizo basi timu hii haimfai.” Alisema Mathew.

“Kwa wengi wenu humu ni mara ya kwanza ninakutana nanyi sijawahi kushiriki nanyi katika misheni yoyote. Nataka niwaweke wazi mimi hutangulia mbele na wenzangu hunifuata nyuma. Hata katika jambo hili nililoliweka mbele yenu sintamtanguliza mbele mtu yeyote,nitatangulia mimi mwenyewe nitawadondosha vibaraka wa mabeberu mmoja baada ya mwingine na baada ya kumaliza kufanya usafi sintakimbia nitajikabidhi

mwenyewe kwa vyombo vya usalama.” Alisema Mathew na wote wakamtazama kwa mshangao.

“Ndiyo maana sikubaliani na mpango huu” alisema Kelvin.

“Mathew huwezi ukafanya jambo kama hilo” alisema Gavana.

“Kuua ni jinai.Baada ya kutenda kosa hilo lazima nijikabidhi mwenyewe kwa vyombo vya sheria ili haki itendeke.Nitafanya hivi kwa

ajili ya kuwalindeni ninyi nyote msiingie katika matatizo.”

“Mathew unafahamu adhabu ya kosa la kuua kwa kukusudia? Ruby aliuliza.

“Ndiyo ninaifahamu. Niko tayari kuibeba lakini kwa wakati ambao nitakuwa ninahukumiwa lazima nchi iwe safi. Yawezekana nikahukumiwa kifo lakini nitakufa nikitabasamu kwa kuilinda nchi. Jamani tusipoteze muda kulijadili hili kuna jambo lingine ambalo

nataka kuliwasilisha kwenu” alisema Mathew na kuwatazama wenzake ambao kauli ile aliyoitoa iliwachanganya.

“Baada ya uchaguzi kusogezwa mbele kufuatia vifo vya wagombea urais, kuna jambo ambalo lazima tulifanye.” Mathew alinyamaza tena kidogo.

“Tunatakiwa kumuondoa Rais aliyeko madarakani.” Nyuso za watu ndani ya kile chumba zilizidi kubadilika na

kuonesha hofu kubwa baada ya kauli ile ya Mathew.

“Mathew nadhani sasa unataka kuvuka mstari.” alisema Gavana.

“Ndiyo mzee. Lazima tuvuke mstari ili nchi yetu iwe salama. Lazima serikali iliyoko madarakani iondoke ili iwe rahisi kufanya usafi na kuondoa mizizi yote ya mabeberu. Hata kama tutasogeza mbele uchaguzi mkuu lakini kama tusipoondoa mizizi yote ya mabeberu

tutakuwa tumefanya mchezo wa kujaza maji kwenye gunia. Bado mabeberu wataendelea na mipango yao.”

“Mathew binafsi sikubalini na huo ni mpango wa uhaini” alisema Kelvin.

“Mathew bado sijakuelewa lengo lako hasa ni nini? Gavana aliuliza.

“Lengo langu ni kuiondoa serikali iliyoko madarakani na kuiweka serikali ya mpito ambayo itafanya usafi mkubwa na kuhakikisha mizizi yote ya

mabeberu inaondolewa. Mpango wangu ni kufanya mapinduzi ambayo yatamuondoa madarakani Rais aliyepo na kuunda serikali ya mpito ambayo itafanya kazi ya kuondoa uozo wote na kukata mizizi yote ya mabeberu. Kuondoa wawekezaji na makampuni yote ya kinyonyaji hapa nchini. Kufuta vyama vyote vya siasa vinavyofadhiliwa na mabeberu, kutengeneza sheria mpya ya kuanzisha na kuendesha

vyama vya siasa ambayo itaruhusu ukaguzi wa kina wa mara kwa mara kujiridhisha kuwa vyama vya siasa haviwi uchochoro wa mabeberu kupita. Hatua hizo hazitawafurahisha mabeberu hivyo watakunjua makucha yao kutaka kuiadhibu Tanzania lakini huo utakuwa ni wakati wetu wa kuwaonesha kuwa tumeamua kulinda uhuru wetu kama nchi na hatutaki kuingiliwa au kupangiwa chochote na taifa lingine liwe

kubwa au dogo. Ni kwa kuchukua hatua hizo ndipo tutaheshimika kama nchi.” alisema Mathew.

“Mathew mawazo yako ni mazuri lakini yataitumbukiza nchi hii katika janga kubwa. Hatuwezi kupambana na hawa wakubwa. Wameshika uchumi wetu na wakiamua kutuadhibu hatuna uwezo wa kupigana nao. Zipo baadhi ya nchi za Afrika ambazo zilijaribu kutunishiana misuli na mataifa makubwa matokeo yake sote

tunayajua. Nashauri itafutwe njia nyingine ya kuendesha mapambano na si kwa mipango hii ya Mathew. Itatuletea hasara kubwa badala ya faida” alisema Lucy.

“Tunawahitaji mataifa ya nje lakini kwa sasa tunatakiwa kuanza kupunguza mazoea nao. Ni wakati wa kuamua kufanya mambo sisi wenyewe kama nchi ambayo ninaamini ni njia salama zaidi ya kukuza uchumi wetu kuliko kuwategemea hawa wezi wa

rasilimali zetu. Hawatupendi wala hawaipendi Afrika.Wanachokipenda ni utajiri wetu pekee. Wakati umefika wa kujenga uwezo wetu wa ndani. Tuimarishe sekta ya afya kwa kujenga hospitali kubwa zenye vifaa na wataalamu wa kutosha, tuimarishe mfumo wetu wa elimu ambao utawawezesha vijana wetu kujiajiri na kuajirika katika viwanda vya ndani. Tujenge taifa la kizalendo lenye vijana watiifu

kwa jamii na nchi yao. Wanasiasa wetu wamekuwa ni vinara wa kuwasemea na kuwafurahisha mabeberu. Hawa si ndugu zetu. Wanachukua mali zetu na kutokomea kwao wakituacha tukiogelea katika umasikini mkubwa. Ndege zinapishana angani zimebeba mali zetu. Meli zinapishana majini zimejaza mali zetu. Ni wakati wa kuamka na kuwaambia imetosha. Hakuna wa kuwatamkia neno hilo zaidi

yetu sisi hapa na tutaweza kutamka hivyo kwa kuiondoa madarakani serikali iliyoko sasa.” Alinyamaza akawakata jicho wenzake kama walimuelewa. Maneno yale yalionekana kuwaingia. Akaendelea.

“Mapinduzi yakifanyika tutamtafuta mtu mzalendo ambaye ataongoza serikali ya mpito, mtu jasiri asiyeogopa ambaye atayafanya haya niliyoyaeleza. Mtu huyo si mwingine ni wewe Gavana”

“Mimi? Aliuliza Gavana kwa mshangao.

“Ndiyo mzee. Wewe ni mmoja wa viongozi waadilifu kabisa waliobaki katika serikali hii. Wengine wengi tayari wameingia katika kitabu cha mabeberu.Unaweza na unastahili kuongoza serikali hiyo ya mpito ninayoizungumza hapa.”

“Mathew umezungumza maneno mazito sana ambayo hata mimi ninayaunga mkono. Tanzania ina bahati kubwa

kuwa na vijana wazalendo kama wewe. Ahsante pia kwa kuniona ninafaa kuongoza serikali. Hata hivyo nchi hii hapa ilipofika inapaswa kuongozwa na kijana kama wewe Mathew Mulumbi. Ni sisi wazee ndio tulioiharibu na kifikisha nchi hapa ilipofika. Ni wakai wenu vijana kuleta mabadiliko. Mapinduzi unayoyazungumza yakifanikiwa ninapendekeza Mathew Mulumbi uwe Rais hata kwa miezi sita tu naamini

haya yote uliyoyatamka utayatekeleza vyema.” Alisema Gavana.

“Mzee uko sahihi kabisa. Hata mimi ninakubaliana na mawazo yako kuwa endapo mapinduzi hayo yatafanikiwa basi Mathew Mulumbi awe Rais wa mpito kuhakikisha anafanya usafi mkubwa hapa nchini. Ana sifa zote” alisema Gosu Gosu.

Mawazo ya Gavana yalikubaliwa na kila mtu mle ndani.

“Ndugu zangu kama nyote mmeridhia kwa moyo mmoja niwe kiongozi wa mpito baada ya mapinduzi mimi sina tatizo. Hata hivyo bado dhamira yangu ya kujisalimisha kwa vyombo vya ulinzi na usalama kwa mauaji ambayo nitayafanya iko pale pale. Hayo ya mapinduzi tutapata nafasi kubwa ya kuendelea kuyajadili lakini kwa sasa tujikite katika awamu ya kwanza ya mpango wetu yaani kuzuia uchaguzi mkuu usifanyike katika tarehe

iliyopangwa.” Alinyamaza kidogo kwa sekunde chache halafu akasema.

“Mgombea wa kwanza kabisa ambaye tunatakiwa kumuondoa ni kutoka chama cha ukombozi wa Afrika. Mtu wa pili ambaye naye anatakiwa kuondolewa ni Israel Maungwana. Huyu ni mtu hatari sana. Ana kundi lake la Kumi 255 ambalo limejiandaa kuchochea vurugu kubwa nchini kama chama chake hakitashinda uchaguzi. Baada

ya kuwaondoa hawa wawili utaibuka mgogoro baina ya makundi yanayowania kushinda uchaguzi na yawezekana kundi la bilionea Camilla likahusishwa na mauaji hayo.Wakati wakiendelea kutafuta mchawi sisi tutaendelea kuwaondoa mmoja baada ya mwingine na watakaposhituka, tayari mapinduzi yatakuwa yamefanyika na nchi itakuwa katika mikono ya wazalendo” alisema Mathew.

NDUGU MSOMAJI,

MATHEW MULUMBI ANAIFANANISHA TANZANIA NA SWALA MNONO KATIKATI YA KUNDI LA MBWA MWITU WENYE NJAA KALI. MABEBERU WENYE NJAA YA RASILIMALI, WANAPIGANA VIKUMBO KUTAFUTA NAFASI YA KUMUWEKA MADARAKANI KIBARAKA WAO NCHINI TANZANIA ATAKAYEWAWEZESHA

KUVUNA UTAJIRI KUBWA. VIJANA WAZALENDO WAKIONGOZWA NA MATHEW MULUMBI WANAKUBALI KUUNGANA ILI KUHAKIKISHA WANAIOKOA NCHI ISIANGUKIE KATIKA MIKONO YA MABEBERU.

MATHEW MULUMBI, PAPI GOSU GOSU, RUBY RAFAEL, AMBOLA, JACLINE MO, JULIUS MUKOKE, REGINA, JOMBAA, JOSEPH TSHIBANGA, GAVANA

JACKSON MZUMILE, LUCY MZUMILE NA KELVIN MZUMILE. WOTE HAWA WANAKUTANA NDANI YA MISHENI MOJA KUHAKIKISHA MABEBERU HAWAFANIKIWI.

JE WATAFANIKIWA?

USIKOSE AMBOLA MSIMU WA PILI.

JIANDAE KWA RIWAYA HIZI ZA MATHEW MULUMBI 2021

AMBOLA II

DEAR MATHEW MULUMBI

MWAMBA

SCANDAL II

KOVID 21

BADO KITABU HIKI KINAPATIKANA.

WASILIANA NASI

